# Nipashe

Jumamosi Oktoba 19, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580053

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




## Vigogo Tucta wasimamishwa madai ubadhirifu wa fedha, kuuza nyumba

UKURASA 3




UKURASA 13

# Msako mkali wizi kompyuta za DPP

• **Polisi** waongeza nguvu ufuatiliaji, wataka wahusika wajisalimishe vinginevyo... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### MILIONI 19.7 KUPIGA KURA UCHAGUZI MITAA

WATU milioni 19.7 86 wamejitokeza kujiandikisha katika daftari la orodha...

UKURASA WA 3

### AJINYONGA NA KUFA KWA MADAI ANA VVU

MKAZI wa kijiji cha Kakoma, Nkasi mkoani Rukwa, Shija Lutonja (23), amejinyonga...

## Muuguzi tuhuma ubakaji apokwa leseni

UKURASA 3



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akipita kwa tahadhari pembeni ya nyumba ambazo zipo hatarini kubomoka kutokana na mmomonyoko wa ardhi katika eneo la Tandale, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store


## Chalamila atangaza wasiooa, wasioolewa kuchapwa viboko

UK. 2


**MICHEZO** NIYONZIMA KIMEELEWEKA YANGA UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Msako mkali wizi kompyuta za DPP

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi nchini limesema limeongeza nguvu nchi nzima kufuatilia wizi wa kompyuta katika ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na kuwaonya wanaohifadhi vitu vya wizi kuwa wakibainika watashukiwa kama mwewe.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusiana na wizi huo, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Missime, alisema wameamua kuongeza nguvu katika kufuatilia wizi huo ambao umeibua maswali kadhaa kila kona.

Juzi, Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, aliliambia gazeti hili kuwa ofisi yake ilipokea taarifa za wizi huo Jumanne asubuhi na wanaendelea uchunguzi huku akisema hakuna anayeshikiliwa.

Jana, Mambosasa alipotumiwa ujumbe mfupi wa maandishi kwa njia ya simu. Alisema uchunguzi wa tukio hilo ili kuwabaini wahusika bado unaendelea.

Mambosasa alisema hadi jana hakuna mtu aliyekuwa amekamatwa kutokana na tukio hilo pia hakutaja idadi ya kompyuta zinazodaiwa kuibwa.

Hata hivyo, Missime alisema taarifa ya Kamanda Mambosasa, inajitosheleza na wanaamini kwa uwezo mkubwa wa watendaji wake watapata ukweli na kukamata wahusika.

"Kwa taratibu zetu za utendaji kazi taarifa hiyo imeshasambazwa nchi nzima na maeneo mengine ili kuongeza nguvu ya ufuatiliaji.

"Tahadhari kwa wenye tabia ya kupokea au kuhifadhi mali za wizi badala ya kufanya hivyo watoe taarifa polisi, la sivyo wakibainika polisi watawashukia kama mwewe anavyoshukia vifaranga vya kuku," alisema Missime.

DPP alipopigiwa simu yake ya mkononi kuhusu tukio hilo na idadi ya kompyuta zinazodaiwa kuibwa, alisema yuko kwenye kikao na jana alipotafutwa simu yake ilikuwa ikiita bila majibu.

Kwa mujibu wa chanzo cha Nipashe, Oktoba 15, mwaka huu, asubuhi ilibainika kuibwa kwa kompyuta hizo.

Moja ya kesi zilizoko katika hatua ya makubaliano ni ya uhujumu uchumi inayowakabili vigogo wa IPTL, Harbinder Sethi na James Rugemarila, wanaodaiwa kutakatisha zaidi ya Sh. bilioni 309.

Watuhumiwa wengine ni mwandishi wa habari za uchunguzi, Erick Kabendera, anayetuhumiwa kukwepa kodi na kutakatisha jumla ya Sh. milioni 173.

Mtuhumiwa mwingine ni Yusuf Ally, maarufu Mpemba wa Magufuli, anayetuhumiwa kusafirisha nyara za serikali zenye thamani zaidi ya Sh. milioni 200.

Aisha, mwandishi wetu alipomtafuta DPP Biswalo Mganga kwa njia ya simu zaidi ya mara 10 hakupokea simu yake.

Oktoba 17, Kamanda Mambosasa aliliambia gazeti hili kwamba Oktoba 15, mwaka huu, kompyuta ambazo haijafahamika idadi yake ziliibwa ofisi ya DPP na watu wasiojulikana.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamanda Mambosasa kwa njia ya simu alikiri kutokea tukio hilo na kwamba jeshi lake linaendelea na uchunguzi.

**Imeandikwa na Romana Mallya na Hellen Mwango**




Wabeba mizigo wakiwa wamening'inia juu ya matoroli yao, wakati wakisubiri wateja nje ya Stendi ya Mabasi ya Mikoani ya Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# RC atangaza kuwachapa viboko mabachela

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameibuka na jambo lingine kutishia kuwacharaza viboko waliofikisha umri wa kuoa na kuolewa lakini bado wako nyumbani.

Kiongozi huyo anatoa kauli hiyo, wiki chache baada ya kuwacharaza viboko wanafunzi waliodaiwa kuchoma bweni la Shule ya Sekondari Kiwanja, wilayani Chunya.

Calamila aliyasema hayo juzi katika kijiji cha Godima wilayani Chunya na kueleza kuwa, wameanza kutumia bakora kwa kila jambo hata wakikuta mtu amekaa nyumbani haolewi wala kuoa.

"Hata tukikuta umekaa pale nyumba huolewi ni bakora tu. Nenda katafute mume muda wako wa kukaa hapo umetosha.

"Tumekuona umekaa hapo nyumbani hujaoa, ni bakora tu. Nenda katafute mke, kuna umri ambao unatosha lazima uchangamshwe, kwa hiyo viboko vinasaidia," alisikika katika video iliyorekodiwa katika mtandao wa kijamii wa 'Youtube'.

Alisema hata baba na mama wakikosana bila watoto kuwaona wakijifungia ndani, wachapane wamalizane huko.

"Mkitoka nje mnasema kwa kweli kila mmoja anapukuta machozi mtoto haoni," alisema.

Oktoba 3, mwaka huu, mkuu huyo wa mkoa alitembelea Shule ya Sekondari Kiwanja na kuwachapa viboko wanafunzi 14 wanaodaiwa kuchoma moto mabweni mawili ya shule hiyo.

Akiwa shuleni hapo na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Chalamila alichukua fimbo na kuwachapa wanafunzi hao, kitendo ambacho kilizua mjadala katika mitandao ya kijamii.

Oktoba Mosi, mwaka huu, mabweni hayo yaliyokuwa yakikaliwa na wanafunzi 150, yaliteketea kwa moto huku wanafunzi wakidaiwa kuhusika.

Siku nne baadaye, Rais John Magufuli akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani Songwe, alimpongeza Chalamila kwa kuwachapa wanafunzi hao na kuagiza wote wafukuzwe shule.

Akizungumza na wananchi, Rais Magufuli alisema alimpigia simu mkuu huyo wa mkoa na kumpongeza.

"Leo (Oktoba 3) nilikuwa naongea na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, nikamwambia ninakupongeza kweli kweli kwa kuwatandika wale viboko, nikamwambia uliwatandika viboko vichache.

"Haiwezekani serikali tunatoa mabilioni (ya shilingi) kujenga madarasa na shule halafu mtoto anakwenda kuichoma, nikamwambia hao watoto fukuza wote, kwa hiyo kidato cha tano na sita wa shule ile wote wamefukuzwa na bodi imevunjwa kwa sababu huo ni uzembe wa bodi ya shule," alisema.

## Milioni 19.7 kupiga kura uchaguzi mitaa

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WATU milioni 19.7 86 wamejitokeza kujiandikisha katika daftari la orodha ya wapiga kura kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa watu hao ni sawa na asilimia 86 ya lengo lililowekwa.

Huku idadi hiyo ya watu wakijitokeza, Jafo alisema Mkoa wa Dar es Salaam ndio umekuwa kinara kwa kuandikisha watu milioni 2.9 sawa na asilimia 108.

Jafo alisema Tamisemi iliweka lengo la kuandikisha watu milioni 22.9 ambao walikuwa na sifa za kupiga kura lakini waliojitokeza ni hao pekee.

Jafo alisema mafanikio hayo yametokana na hamasa kubwa iliyofanywa na viongozi wa kitaifa, Tamisemi, mikoa, wilaya, halmashauri, tarafa, kata hadi ngazi ya vitongoji na wasanii.

Waziri huyo alitaja mikoa mingine kuwa na idadi kuwa ni Pwani (568,627 asilimia 96), Mwanza (1,340,177 asilimia 95), Tanga (983,104 asilimia 90), Singida (610,344 asilimia 90), Morogoro (1,075,379 asilimia 89), Mbeya (776,811 asilimia 88), Ruvuma (651,257 asilimia 88), Katavi (234,163 asilimia 88) na Mtwara (604,670 asilimia 86).

Mingine ni Dodoma (893,890), Rukwa (410,760) na Arusha (787,232) yote asilimia 85 kila mmoja, Lindi (396,832), na Iringa (433,259) asilimia 84 kila mmoja, Mara (673,065 asilimia 80), Kilimanjaro (741,130), Geita (664,100) na Manyara (565,827) asilimia 79.

Tabora (879,664), Songwe (402,840) na Kagera (961,520) asilimia 78, Shinyanga (583,928) na Simiyu (568,342) asilimia 76, Njombe (260,791) asilimia 75 na Kigoma (676,012) asilimia 65.

HABARI KITAIFA

# Vigogo Tucta wasimamishwa kazi

**Na Mary Geofrey**

SHIRIKISHO la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (Tucta), limewasimamisha kazi Katibu Mkuu wake, Dk. Yahya Msigwa na Naibu wake, Jones Majura, kwa tuhuma za ubadhilifu wa fedha na matumizi mabaya ya madaraka ikiwamo kuuza nyumba.

Rais wa Tucta, Tumaini Nyamhokya, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, alithibitisha kusimamishwa kazi kwa watendaji hao wakuu ili kupisha uchunguzi dhidi ya tuhuma zinazowakabili.

"Wamesimamishwa kazi kwa lengo la kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili, kikao cha kamati ya utendaji kiliwataka kukaa pembeni," alisema Nyamhokya.

"Tumewasimamisha kazi kwa muda ili kupisha uchunguzi na kuona hatua zinazofuata na hatujawafukuza," alisisitiza.

Alipoulizwa kuhusu tuhuma zinazowakabili alisema: "Hayo ni mambo ya kikao cha ndani ni masuala la kamati ya utendaji ya shirikisho, tuhuma zikibainika ndipo tutawajulisha ila ni mambo ya ndani."

Taarifa za awali zilizolifikia gazeti hili zilisema viongozi hao walisimamishwa kazi wiki iliyopita ili kupisha uchunguzi dhidi ya tuhuma zinazowakabili ikiwamo kuuza nyumba ya shirikisho iliyoko Mafinga mkoani Iringa.

Nyamhokya alisema viongozi hao wanadaiwa kuuza nyumba hiyo bila uamuzi wa vikao halali vya shirikisho na bila kufanya tathmini ya jengo lenyewe.

Taarifa za uchunguzi dhidi ya tuhuma hizo, kwa mujibu wa taarifa za ndani za Tucta, zitapelekwa Baraza Kuu na Mkutano Mkuu utakaofanyika baadaye mwezi huu ili kutoa uamizi.

"Vikao vitakavyofanyika ndivyo vitaamua hatima yao kama warudishwe kazi au wafukuzwe kabisa," kilieleza chanzo hicho.




Mafundi wakiendelea na kazi ya kujenga vituo vya daladala, katika Barabara ya Sinza Kijiweni-Tandale, katika eneo la Tandale, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Muuguzi afungiwa leseni tuhuma kubaka mgonjwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BARAZA la Uuguzi na Ukunga Tanzania, limemfungia kutoa huduma za uuguzi na ukunga Damian Mgaya kwa miezi mitatu kutokana na tuhuma za kumbaka binti wa miaka 16 baada ya kumchoma sindano ya usingizi.

Aidha, vyombo vya dola vimeombwa kumsaka na kumkamata mtuhumiwa huyo ili aweze kujibu tuhuma zinazomkabili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msajili wa Baraza hilo, Agnes Mtawa, muuguzi huyo anadaiwa kutenda kosa hilo Oktoba 9, mwaka huu, katika Hospitali ya Wilaya ya Igunga mkoani Tabora. Mtawa alisema Mgaya anatuhumiwa kufanya kitendo hicho kwa binti aliyekuwa akimuuguza mama yake mzazi hospitalini hapo baada ya kumchoma sindano ya usingizi.

"Baraza limemfuatilia muuguzi huyo na kubaini ametoroka kituoni hapo, hivyo tunaomba vyombo vya ulinzi na usalama vimsake popote alipo akamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria ili ajibu tuhuma zinazomkabili," alisema.

Kutokana na tuhuma hizo, alisema kwa mamlaka ya baraza hilo, kwa Sheria ya Uuguzi na Ukunga, anasimamishiwa leseni yake ya kutoa huduma za uuguzi na ukunga popote nchini kwa muda wa miezi mitatu wakati taratibu za uchunguzi zikiendelea.

Alieleza kuwa iwapo itathibitika alifanya kitendo hicho, hatua za kisheria zitachukuliwa.

Alitoa wito kwa wauguzi na wakunga popote nchini kufanya kazi kwa weledi na kutoa huduma kwa kuzingatia taratibu, sheria na kanuni.

Msajili alisema muuguzi huyo tukio hilo si la kwanza kufanya hivyo na kwamba mwaka 2017 alitenda kosa la aina hilo katika kituo cha afya Iguruki wilayani Igunga na kupelekwa polisi na kisha kufikishwa mahakamani na kufunguliwa kesi lakini mwaka 2018 mahakama ilimuachia huru.

Uongozi wa afya wilayani Igunga baada ya mtumishi huyo kurejeshwa kazini, ulimhamishia katika Hospitali ya Wilaya Igunga.

# Ajinyonga na kufa kwa madai ana VVU

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MKAZI wa kijiji cha Kakoma, Nkasi mkoani Rukwa, Shija Lutonja (23), amejinyonga huku akiacha ujumbe kuwa haoni sababu ya kuishi kwa kuwa ana virusi vya Ukimwi (VVU).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Richard Kandege, mwanamke huyo alikutwa amejinyonga kwenye mti kwa kutumia kanga.

Alisema mwanamke huyo alichukua uamuzi wa kujinyonga juzi kati ya saa 3:00 na saa 4:00 asubuhi na aligundulika amejinyonga baada ya watu waliokuwa wakipita katika maeneo hayo kuona mwili ukining'inia juu ya mti na kutoa taarifa kwenye ofisi ya kijiji.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Patrick Mwami, alisema baada ya tukio hilo, walitoa taarifa polisi ambao walifika eneo la tukio na katika uchunguzi wao hawakuona majeraha yoyote katika mwili wake zaidi ya yale ya kujinyonga.

Alisema katika mwili wa marehemu walikuta ujumbe mfupi wa maneno aliouandika kuwa ameamua kujiua kwa sababu amepimwa na amekutwa na VVU lakini pia mume wake amefungwa jela hivi karibuni, hivyo haoni sababu ya kuendelea kuishi duniani

Mwenyekiti huyo alisema tukio hilo limeacha simanzi kubwa katika kijiji hicho kwa kuwa ni mara ya kwanza kwa mwanamke kuchukua uamuzi kama huo kujinyonga hadi kufa.

Mkuu wa Wilaya Nkasi, Said Mtanda, amethibitisha kutokea kwa kifo hicho na kuitaka jamii kuacha kujichukulia sheria mikononi wakati jambo lake lilikuwa la kawaida kwa kuwa si yeye peke yake mwenye VVU.

# Vigogo Chadema kuanza kujitetea wenyewe

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imekubali pingamizi la Jamhuri kwamba vigogo tisa akiwamo Mwenyekiti Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, kuanza kujitetea wao wenyewe kabla ya mashahidi kutoka nje katika kesi inayowakabili dhidi ya uchochezi.

Uamuzi huo ulitolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Hakimu alisema baada ya kusikiliza hoja za pande zote pamoja na vifungu vya sheria vilivyowasilishwa, mahakama yake imeona pingamizi la awali la Jamhuri lilikuwa na mashiko ya kisheria.

Alisema mahakama yake iliwaona washtakiwa wana kesi ya kujibu na matakwa ya sheria yanaelekeza mshtakiwa kuanza kujitetea dhidi ya mashtaka yake ikiwamo kusomewa upya mashtaka na kumpatia haki zake.

"Mahakama hii baada ya kupitia hoja za pande zote mbili imekubaliana na pingamizi la awali la Jamhuri kwamba kisheria washtakiwa wanatakiwa kuanza kujitetea na mashahidi wao watafuata kutoa ushahidi wao dhidi ya Jamhuri," alisema Hakimu Simba wakati akitoa uamuzi huo mdogo.

Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, alidai wamekubaliana na uamuzi wa mahakama, lakini wanaomba muda wa kutosha wa kuwaandaa washtakiwa hao.

Alidai washtakiwa wote tisa watajitetea na kwamba wameandika barua kuomba vielelezo vinne ikiwamo CD ya video inayoonyesha picha za tukio la maandamano, lakini mpaka sasa hawajapata.

Hakimu Simba aliahirisha kesi hiyo hadi Oktoba 21, mwaka huu, kwa ajili ya kutoa uamuzi kama washtakiwa wapewe wiki tatu za kujiandaa kutoa ushahidi au la.

Mbali ya Mbowe, washtakiwa wengine ni, Katibu Mkuu Taifa, Dk. Vicent Mashinji, Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, Katibu Mkuu Taifa, Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Mbunge wa Tarime vijijini, John Heche, Mbunge wa Iringa mjini, Peter Msigwa na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Wengine ni, Mbunge wa Tarime Mjini, Ester Matiko na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kula njama, wote wanadaiwa kuwa, Februari mosi na 16, mwaka jana, jijini Dar es Salaam, waliku a njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko kutawanyika.


**KUPOTEA KWA CHETI**



115467002

**Francisca John Kihengele** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **P.0741/0511** iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2019 katika Shule ya Sekondari Itende.Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/CEN/RB/380741/2019**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;205/2019**

**Ombi la OMARY SIMBA MOHAMED Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SELUNGWI ZABRONI UBWE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 21/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/10/2019



115467502




Kamishna Jenerali wa Magereza nchini, Phaustine Kasike akiangalia chumvi inayozalishwa na kiwanda cha Gereza la Mtwara akiwa katika ziara yake ya kikazi, mkoani humo, juzi. **PICHA: MAGEREZA**

# Ndalichako aikunjulia kucha Suma JKT

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amelijia juu Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (Suma-JKT) kwa kushindwa kujenga kwa wakati na kutotoa gharama halisi za ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga, Kasulu mkoani Kigoma.

Pia ametoa siku 15 kwa mshauri elekezi ambaye ni BICO iliyo chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kufanya tathmini ya gharama za ujenzi wa chuo hicho kwa kuwa zinatia shaka.

Alisema kwa haraka haraka kujenga majengo madogo ambayo aliyaita kuwa ni ghorofa mtoto, haiwezi kujengwa kwa Sh. bilioni 10.

"Hizi gharama nilishazikataa toka mwanzo, nawapa muda hadi Oktoba 30, mwaka huu, nipate taarifa sahihi,"alisema.

Waziri huyo alisema licha ya kupewa fedha, kazi haiendelei vizuri na kwamba hakuna nguvu kazi wala vifaa vya kutosha.

"Nimekupa hela ili ufanye kazi, kwa nini mnabania hela? Msingi mmechimba toka mwezi wa saba (Julai) na hakuna nguvu kazi. Idadi ya wafanyakazi waliopo hapa ni wa kujenga kibanda cha kuku,"alisema.

"Nyumba ya serikali ya Sh. bilioni 10 idadi ya watu walioko kwenye kazi haitoshi. Hii ni sawa na mtu anajenga nyumba yake ya Sh. milioni 20 unakua na mafundi watano au sita," alisema na kuongeza:

"Askari hutakiwi kuwa mbishi unatakiwa kupokea na kutekeleza, ukiwa mbishi namna hii kazi haiwezi kwenda, unatetea nini unaona watu hawa wanatosha kufanya hii kazi na kukamilika kwa wakati?kila jengo lilitakiwa liwe na mashine yake lakini hapa naona mashine moja."

Alisema walichagua Suma JKT ili kazi ifanyike vizuri na ikamilike mapema lakini kwamba kasi ya kazi hairidhishi kabisa huku mvua zikikaribia kuanza.

"Eneo la ujenzi lenye thamani ya Sh.bilioni 10 kuna mashine moja ya kuzunguka ambayo ni sawa na kujenga kibanda cha kuku. Ilipaswa kuwa na vifaa vya kutosha. Fedha zipo na ninataka kazi ikamilike watoto wasome

**INAENDELEA UK. 8**

# Benki ya Dunia yaimwagia Zanzibar bil. 340/-

**Na Waandishi Wetu,**
WASHINGTON DC

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar inatarajia kupata dola za Marekani milioni 150 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo kukuza Utalii na ustawishaji miji.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar, Khamis Omar, alisema jijini hapa jana kuwa Benki ya Dunia imekuwa mshirika mzuri wa maendeleo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutokana na misaada mbalimbali inayoitoa katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Omar alisema benki hiyo imefadhili ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwamo ya barabara zinazoingia mijini, Uwanja wa Ndege wa Zanzibar na bandari.

Aidha, alisema benki hiyo imesaidia ujenzi wa uwanja wa ndege kwa kujenga sehemu ya maegesho ya ndege, njia ya kutua na kurukia ndege na njia ambazo ndege zinapita kabla ya kuingia kwenye sehemu ya kurukia.

"Pia Benki hii imekuwa ikisaidia miradi mbalimbali ya elimu Zanzibar ukiwamo mradi wa kukuza matokeo na kuongeza ufaulu wa wanafunzi katika shule za Zanzibar," alisema Omar.

Katibu mkuu huyo alisema kwa sasa wanatekeleza mradi mkubwa wa ustawishaji wa huduma za mijini ambao unafadhaliwa na benki hiyo ambao utasaidia kuboresha huduma muhimu katika miji ya Zanzibar na kuongeza vivutio vya utalii.

"Mradi huu umekamilika katika awamu ya kwanza na awamu ya pili itatekelezwa baada ya benki hiyo kuridhia na kutoa idhini ya utekelezaji wa mradi huo. Idhini hiyo inatarajiwa kutolewa Aprili, mwakani," alisisitiza.

Kutokana na msaada huo, aliishukuru Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ushirikiano wanaouonyesha katika kusukuma maendeleo ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Awali, Waziri wa Fedha na Mipango wa Zanzibar, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, alisema lengo la kushiriki katika mikutano ya mwaka ya Benki ya Dunia na IMF ni kujadiliana na vyombo hivyo vya fedha duniani kuhusu miradi inayotekelezwa kwa sasa na kuangalia mustakabali wa utekelezaji wa miradi ambayo inatarajiwa kutekelezwa baadaye.

HABARI KITAIFA

# Waziri aagiza upimaji shamba hekta 2,000

**Na Munir Shemweta, UKEREWE**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kupima na kupatiwa hati shamba lake la miti la Rubya, wilayani Ukerewe lenye ukubwa wa hekta 1,926.3.

Dk. Mabula alitoa agizo hilo juzi wakati alipokwenda kukagua ujenzi wa nyumba za watumishi wa TFS unaofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) akiwa katika ziara ya siku moja katika kisiwa cha Ukerewe kufuatilia utendaji kazi wa sekta ya ardhi katika hamashauri za mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Alisema kinachohitajika sasa kwa TFS ni kuhakikisha shamba hilo linapimwa na kupatiwa hati itakayoonyesha mipaka halisi ili kuepuka migogoro.

"Miji inakua na wananchi bado wanahitaji maeneo. Bila kuwa na hati inayoonyesha mipaka ya shamba kunaweza kuleta migogoro. Tuelewe hati inalinda mipaka ya shamba lisivamiwe na wananchi," alisema.

Naibu Waziri pia aliagiza eneo la shamba kuwa mpango kina utakaoonesha kila matumizi ya sehemu ya ardhi kwa kuwa katika eneo hilo mbali na shamba la misitu kuna makazi ya watu.

Meneja wa Shamba hilo, Festo Chaula, alimweleza Naibu Waziri Rubya ni miongoni mwa mashamba 23 yanayomilikwa na TFS lililoanzishwa mwaka 1951 kwa Tangazo la Serikali Namba 230.

Alisema wakala pia ina eneo lingine lilipandwa miti kwa ubia na halmashauri ya wilaya ya Ukerewe lenye ukubwa wa hekta 1,152 lenye miti aina ya misindano.

Kwa mujibu wa Chaula, katika kuboresha makazi ya watumishi wa wakala, Sh. milioni 383.8 zimetengwa katika mwaka wa fedha wa 2019/20 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tatu, tangi la kuhifadhia maji, ukarabati wa nyumba mbili na ujenzi wa uzio wa bustani ya miti, kazi ambayo ilianza Agosti, mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Dk. Mabula ameiagiza halmashauri ya wilaya ya Ukerewe kupima maeneo katika halmashauri hiyo kama operesheni maalum ili kuondoa migogoro ya ardhi sambamba na kuondoa ujenzi holela.

Akizungumza na madiwani pamoja na watumishi wa ardhi katika halmashauri hiyo, Dk. Mabula alisema halmashauri hiyo ina vifaa vya upimaji, hivyo kinachotakiwa kwa sasa ni kuwasiliana na ofisi ya Ardhi Kanda ya Ziwa kwa ajili ya kupatiwa



Mwendesha pikipiki iliyosheheni magunia ya mkaa, akiifanyia matengenezo baada ya kuharibika katika eneo la Chanika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ashikiliwa tuhuma mauaji ya mdogo wake

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma, linamshikilia Mohamed Luambano (70) mkazi wa Mtelamwai wilayani Namtumbo kwa tuhuma za kumkata na kitu chenye ncha kali kichwani na kiganja cha mkono wa kulia mdogo wake, Abeid Luambano (65) na hatimaye kufariki dunia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alisema tukio hilo limetokea juzi majira ya saa 2:00 usiku katika kitongoji cha Doroba kilichoko katika kijiji cha Mtelemwai.

Alisema inadaiwa siku ya tukio, Abeid alikutwa akiwa ameuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali na pia kukatwa kiganja cha mkono wa kulia na watu wasiofahamika.

Maigwa alisema Abeid kabla ya kuuawa, alivamiwa ghafla na watu wasiojulikana nyumbani kwake na kisha kutolewa nje ya nyumba yake na kuanza kupigwa na kitu chenye ncha kali hadi kupoteza maisha.

Kutokana na tukio hilo, alisema Luambano ambaye ni kaka wa marehemu, amekamatwa kwa mahojiano zaidi kutokana na madai kwamba siku za karibuni kumekuwapo na kutoelewana kati ya ndugu hao.

Alisema ugomvu huo ulisababishwa na Abeid kuchomewa nyumba yake aliyokuwa akiishi akimtuhumu kaka yake na mtoto wake aliyetajwa kwa jina la Msajiri kuwa walikuwa wakimfanyia vitu vibaya.

Mtoto huyo wa Luambano amekimbia na kutokomea kusikojulikana baada ya tukio hilo la mauaji. Kamanda maigwa alisema juhudi za kumtafuta zinaendelea.

Katika tukio lingine, Nuru Milanzi, mfanyabiashara mdogo na mkazi wa Mashujaa, Manispaa ya Songea, amekutwa akiwa amefariki dunia baada ya kujinyonga kwa kutumia kamba ya manira ndani ya chumba alichokuwa analala.

Kamanda Maigwa alisema tukio lilitokea juzi majira ya saa 1:00 usiku baada ya Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mashujaa, kutoa taarifa kituo cha polisi kuwa Milanzi amekutwa nyumbani kwake akiwa amejinyonga na kufariki dunia.

Alisema chanzo cha kujinyonga kwake inadaiwa ni madeni yaliyokithiri kwenye vicoba ambayo yalimsababishia msongo wa mawazo.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF iwe makini mrithi wa Wambura TPLB

**JUMANNE** wiki hii, Shirikikisho la Soka nchini (TFF), lilitangaza rasmi kuwa kesho yake [Jumatano], litaanza mchakato wa kumtafuta Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), kufuatia aliyekuwa akikalia nafasi hiyo, Boniface Wambura, kumaliza mkataba wake. Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, akitangaza uamuzi huo, alisema Jumatano wiki hii wangeanza kutoa matangazo kwa ajili ya wadau mbalimbali wa soka kuomba nafasi hiyo muhimu kwa ajili ya kuliongoza soka la nchi hii.

Aidha, Wambura ambaye amewahi kuwa mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo Tanzania (TASWA) na baadaye Ofisa Habari wa TFF, amepewa majukumu mengine ambapo sasa atakuwa Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Masoko wa TFF akishirikiana na Clifford Ndimbo katika upande wa habari wakati Aaron Nyanda, atafanya naye kazi za kutafuta masoko.

Tunampongeza Wambura si tu kwa majukumu mapya aliyopewa, bali kwa changamoto kubwa alizokabiliana nazo wakati akiwa Mtendaji Mkuu TPLB, kwani ni idara ambayo inahitaji umakini mkubwa na uelewa wa kutosha wa masuala ya soka.

Hivyo, tunatumai ataendelea kutoa ushirikiano wa kutosha katika majukumu yake mapya, lakini pia pale mrithi wake katika nafasi ya Mtendaji Mkuu wa TPLB atakapopatikana.

Hata hivyo, kuelekea mchakato mpya wa kumsaka mrithi wa Wambura, tunaitaka TFF kuwa makini na kuifanya kazi hiyo kwa kutumia weledi wa hali ya juu kwani idara hiyo ndiyo mhimili mkubwa wa soka la Tanzania. Kwa muda mrefu klabu, makocha, mashabiki na wadau wa soka kwa ujumla wamekuwa wakilalamikia suala zima la mabadiliko ya ratiba ya Ligi Kuu mara kwa mara, jambo ambalo mara nyingine tumeshuhudia timu moja ikiwa na viporo hadi zaidi ya sita kwa kisingizio tu inashiriki michuano ya kimataifa ambayo kalenda yake hutoka mapema hata kabla ya ile ya Ligi Kuu kupangwa.

Hali kadhalika, msimu uliopita tulishuhudia ukimalizika bila Ligi Kuu kuwa na mdhamini jambo ambalo hadi leo haijajulikana bingwa wa ligi hiyo, Simba atapewa zawadi gani mbali na kombe ambalo walikabidhiwa. Kwa hayo machache tu, bila kuwa na Mtendaji Mkuu wa TPLB, mwenye taaluma ya kutosha atakayeweza kuunda timu yake imara ya kufanya nayo kazi, hakika soka la Tanzania litaendelea kuwa la kujikongoja na itakuwa vigumu kuweza kufikia kule tunapopatamani walipo wenzetu waliopiga hatua kisoka.


Aidha, pamoja na mchakato ambao Nipashe tunaamini TFF itauendesha kwa umakini na weledi wa hali ya juu kabisa bila kutazama itikadi ya vyama, siasa, dini ama klabu kwa manufaa ya soka letu, pia tunataka utakapokamilika na kuiacha Bodi ya Ligi kuwa huru kama ambavyo zinavyofanya nchi za wenzetu zilizopiga hatua kisoka. Tunatambua hata kama TFF itafanikiwa kumpata Mtendaji Mkuu wa TPLB mwenye taaluma ya kutosha na makini katika kazi hiyo, kama hatakuwa huru katika kutekeleza majukumu yake, itakuwa ni kazi bure kwani tutaendelea kuyashuhudia madudu yale yale ambayo hatutamani kuyaona katika soka letu.

Tunaamini Rais wa TFF, Wallace Karia na Katibu wake, Kidao si tu watahakikisha mchakato huo haufanyiki kwa lengo la maslahi yao binafsi, bali watamulika zaidi nani anayeweza kuleta mapinduzi mapya kwenye ligi yetu ikiwa ni pamoja na kuwezesha vyanzo vingi vya mapato vinazidi kupatikana.

Ni aibu kubwa kwa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo tunaamini ni miongoni mwa ligi bora kabisa Afrika Mashariki na Kati na inayotazamwa zaidi, kuwa na wadhamini watatu tu, Kampuni ya Vodacom ambao ni wadhamini wakuu, Benki ya KCB wadhamini wenza pamoja na Azam TV inayodhamini upande wa kurusha matangazo ya mechi. Hivyo, kama TFF itakuwa makini katika kumtafuta Mtendaji Mkuu wa TPLB lakini pia ikatoa uhuru kwake katika kutekeleza majukumu yake, ni wazi tutashuhudia soka letu likipiga hatua kubwa na kuvutia wawekezaji wengi kuliko ilivyo sasa.

Ni matumaini yetu TFF itazingatia hayo tuliyoyaeleza ili kuliinua soka letu hususan Ligi Kuu ambayo kwa sasa imeanza kuwa kivutio kikubwa ndani na nje ya nchi kwa makocha wengi na wachezaji kuvutiwa kuja kufanya kazi nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kongole Jeshi la Polisi Kigoma kwa ulinzi makini uwanjani

**ZIARA** ya Simba mkoani Kigoma imeibua vitu kadhaa vipya ambavyo mashabiki wengi wa soka hasa wa mikoa mingine nchini hawakuwahi kuviona vikitokea hapa nchini.

Simba ilienda Kigoma baada miaka mingi kupita tangu enzi za Mbanga FC ilipokuwa Ligi Kuu na ikacheza na timu za Mashujaa, ikashinda bao 1-0 na mechi nyingine ilikuwa dhidi ya Mabingwa wa Burundi, Aigle Noir na ikatoka nao sare tasa.

Mechi hizo zote zilichezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Kitu cha kwanza ambacho kilishangaza wengi ni mapokezi makubwa iliyoyapata Simba tangu ilipowasili Uwanja wa Ndege na mitaani ambako kulikuwa na umati mkubwa wa mashabiki, uliowavutia mno wachezaji na benchi la ufundi la timu hiyo.

Kilichofuatia kingine ni jinsi mashabiki wa soka Kigoma walivyojitokeza kwa wingi kwenye mechi hizo mbili. Taarifa zinaeleza kuwa, saa nne asubuhi, tayari uwanja ulikuwa umeshaanza kufurika watu kutoka sehemu mbalimbali mkoani humo.

Halafu wakazi wa Kigoma si tu kwamba walikuwa wamejazana uwanjani, lakini walikuwa wakishangilia mno muda wote kitu ambacho huwashinda hata mashabiki wa soka wa Dar es Salaam.

Kitu kingine kilichowashangaza wengi ni ubovu wa Uwanja wa Lake Tanganyika. Nadhani utakuwa unaongoza kwa ubovu kati ya viwanja vyote Tanzania kama sitokosea.

Udongo mwekundu ndiyo unaoonekana zaidi kuliko nyasi. Nyasi chache zilizobaki uwanjani zimekaukiana kwa kukosa maji na rutuba. Kusema kweli sehemu ya kuchezea uwanjani inasikitisha kweli kweli.

Jinsi mashabiki wa Kigoma walivyojitolea kwenye ziara ya Simba na kama kungekuwa na kiwanja kizuri, basi wangefaidi kandanda safi na pesa yao ingekwenda kihalali.

Cha mwisho ni muundo wa ulinzi kwenye uwanja huo. Haijapata kutokea kuona muundo ule wa ulinzi kwenye viwanja vyote nchini Tanzania. Aina ile ya ulinzi mara nyingi huwa tunaiona nje ya nchi kwenye ligi mbalimbali hususan Ulaya.

Kuna baadhi ya watu walidiriki kusema kuwa huenda hawakuwa askari wa Tanzania wanaolinda uwanja huo. Lakini ukweli ni kwamba walikuwa ni Wabongo.

Muda wote walikuwa wamegeukia mashabiki kama Ulaya vile. Walikuwa wameachiana nafasi na kuzunguka uwanja mzima, huku wakitazamana na mashabiki, tofauti na tulivyozoea askari polisi wakiwa nao ni sehemu ya watazamaji wa soka katika viwanja vingine.

Umati mkubwa wa mashabiki Kigoma ulivyokuwa uwanjani na jinsi askari walivyokuwa wanalinda ilivutia mno, kiasi kwamba wengi waliokuwa wanaangalia kwenye televisheni walisifu na kumtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, kuagiza askari wake kote nchini wanaopewa jukumu la kulinda usalama viwanjani wakati wa mechi kuiga mfano ule.

Aina ile ya ulinzi hata kama kunatokea tatizo ni rahisi kulitatua kwa muda mfupi na bila madhara makubwa huku mhusika kama anatokea jukwaani kuwa rahisi kujulikana. Kwa sababu mtu wa kwanza kumpiga mwenzake, kurusha chupa au kufanya fujo ataonekana na kudhibitiwa kwa urahisi.

Lakini askari wanaoangalia soka wanashtukia fujo imeshakuwa kubwa na kinachofanyika nao wanahamaki na kupiga mabomu ya machozi.

Yeyote aliyetoa mafunzo kwa askari polisi wa Kigoma anastahili sifa. Kamanda wa Polisi Mkoani Kigoma na hata ni makamanda wa vituo vya polisi vilivyotoa askari nao pia wanastahili sifa na kuwa mfano kwa wengine. Nadhani askari polisi na walinzi wa viwanja vingine vya soka nchini wanachukujifunza kutoka kwa wenzao wa Kigoma ambao pamoja na kwamba hawana Ligi Kuu kwa miaka mingi, lakini kiulinzi 'wametisha' zaidi na sina budi kutoa kongole kwao.'

HABARI KITAIFA

# Abiria wanusurika kifo basi kuwaka moto

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

Abiria 20 waliokuwa wakisafiri kutoka Shinyanga kwenda Tanga, wamenusurika kifo baada ya basi walilokuwa wakisafiria kuwaka moto, katika eneo la Mhizi, wilayani Shinyanga.

Tukio hilo limetokea jana majira ya 12:30 wakati basi hilo la Freys Coach lenye namba za usajili T 119 BDY likiendeshwa na Msami Atwayi (39) likiwa njiani kwenda Tanga.

Basi hilo lilianza kuwaka moto hivyo kusababisha abiria wote kushuka na kuanza kuuzima moto huo. Hakuna kifo wala majeruhi kutokana na tukio hilo.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Josephine Charles, ambaye ni miongoni mwa abiria hao, alisema walipokuwa njiani walianza kusikia harufu za breki lakini waliendelea na safari ndipo ikatokea Toyota Hiace iliyokuwa nyuma yao na kutoa ishara ili dereva asimamishe gari kwa kuwa matairi yalikuwa yanawaka.

Alisema baada ya dereva kusimama, matairi mawili yalipasuka na basi kuanza kuanza kuwaka moto.

Hata hivyo, alisema abiria wote walishuka na kuanza kuuzima moto kwa kutumia mchaga, huku wengine wakitoa taarifa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambalo lilifika kwa wakati na kuuzima moto huo.

"Baada ya dereva kusimama abiria wote tulikimbilia nje na kuanza kushirikiana kuuzima moto ili usilete madhara makubwa zaidi. Muda mfupi zimamoto walifika na kuuzima kabisa na hakuna kifo wala majeruhi," alisema Charles.

Kamanda wa Polisi Mkoani Shinyanga, Richard Abwao, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha hakuna mtu yeyote aliyepata madhara kwenye ajali hiyo.

Abwao alisema abiria wote waliokuwa katika basi hilo, walishafaulishwa kwenye mabasi mengine na kuendelea na safari.

Aidha alisema chanzo cha ajali hiyo ni hitilafu kwenye mfumo wa breki iliyosababishwa na msuguano na hatimaye kutokea moto na kuanza kuliunguza basi hilo.

Hata hivyo, Abwao alisema basi hilo halikuwaka lote kutokana na abiria kuanza kuzima moto huku jeshi la zimamoto nalo likifika kwa wakati na kuuzima.



Wachuuzi wa viazi mviringo wakiviandaa wakati wakisubiri wateja kando ya Barabara ya Mabibo, eneo la Urafiki jijini Dar es Salaam jana. Ndoo moja ya viazi yenye ujazo wa lita 20 iliuzwa kwa bei ya 9,000/-. **PICHA: JOHN BADI**

# Kioo Ltd yang'ara tuzo uzalishaji bora

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya kutengeneza chupa ya Kioo Limited ya jijini Dar es Salaam, imeibuka mshindi wa wazalishaji wa bidhaa zinazotokana na madini kwa viwanda vikubwa kwenye tuzo za Rais za mzalishaji bora kwa mwaka 2019.

Tuzo hizo zilizoandaliwa na Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI), zilitolewa jana na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kwa niaba ya Rais John Magufuli kwenye hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Meneja Maendeleo na Mafunzo wa Kioo Limited, William Bongo, ndiye aliyepokea tuzo hiyo kwa niaba ya uongozi wa kampuni hiyo.

Akizungumzia siri ya mafanikio hayo, Bongo alielezea kufurahishwa na tuzo hiyo na kueleza kuwa imewapa moyo wa kuendelea kufanya kazi kwa ajili ya jamii ya Watanzania.

Alisema mikataba bora na uhusiano mwema na wafanyakazi wa kampuni hiyo wanaofikia 551, ni baadhi ya vigezo vilivyowapa ushindi huo wa mwajiri bora.

"Tuzo imetupa moyo kwamba kazi zetu kwa jamii zinatambulika hivyo sisi tunawaahidi Watanzania kwamba tutazidi kuboresha huduma zetu na uhusiano na wafanyakazi wetu kwa kuendelea kuboresha maslahi yao," alisema Bongo.

Alisema uhusiano mzuri na wafanyakazi na taasisi mbalimbali umechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya kampuni hiyo kwani hakujawahi kutokea migogoro wala migomo ya wafanyakazi.

Kuhusu uwazi katika ajira za kampuni hiyo, alisema wana kanzidata ya watu waliotuma maombi ya kazi, hivyo kila inapotokea nafasi wanaangalia mwenye sifa zinazotakiwa na kisha kuitwa kwenye usaili.

"Mfano unaweza kukuta mtu alituma maombi mwaka uliopita lakini pale inapotokea nafasi anashangaa kuitwa kwenye usaili na hatimaye anapata kazi. Uwazi unatawala kwenye kuajiri," alisema

Akizungumzia Kioo Ltd inavyoshiriki kwenye shughuli mbalimbali za kijamii, Bongo alisema wana uhusiano mweka na wilaya ya Temeke na wameshiriki shughuli mbalimbali za maendeleo.

"Kila wanapotuomba kushirikiana nao katika suala fulani la maendeleo sisi huwa hatusiti kushiriki na tunawaahidi kuwa tutaendelea kushirikiana nao watakapotuhitaji ili kuleta maisha bora kwa Watanzania," alisema Bongo.

Alisema kampuni hiyo iliingia mkataba wa hali bora na wafanyakazi hali ambayo imekuwa ikiwawezesha kuboresha maslahi ya wafanyakazi mwaka hadi mwaka

# Macedonia yaongoza darasa la saba Ilala

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Macedonia iliyoko Tabata Bonyokwa, imekuwa ya kwanza kwa Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam katika matokeo ya darasa la saba.

Kwenye matokeo hayo yaliyotangazwa hivi karibuni na Baraza la Taifa la Mitihani (Necta), shule hiyo imeshika nafasi ya pili kwa Mkoa wa Dar es Salaam kati ya shule 459 zilizopo.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Benard Josia, alisema juzi kuwa wanafunzi waliofanya mtihani huo walikuwa 102 na 99 walifaulu kwa wastani wa daraja A na wawili tu ndio waliopata daraja B.

Josia alisema shule hiyo pia imeshika nafasi ya 23 kitaifa kati ya shule 9,929 na kuzipita shule kongwe nchini akieleza kuwa hayo ni mafanikio makubwa kwa shule yake.

Alisema wameyafurahia matokeo hayo na kuahidi kufanya vizuri zaidi kwenye mitihani ijayo kwani walimu wamejipanga kufudisha bila kuchoka kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

Mwalimu huyo alisema kwenye matokeo ya mtihani wa moko mwaka huu shule hiyo ilikuwa ya kwanza kwa Mkoa wa Dar es Salaam na wanafunzi wake walifaulu kwa kiwango cha kuridhisha.

Alitaja siri ya mafanikio yao kuwa ni kujiwekea malengo makubwa na kufanya kazi kwa bidii usiku na mchana kwani matokeo mazuri kama hayo hayawezi kuja kwa miujiza.

"Tunajitahidi kujua udhaifu wa mwanafunzi mmoja mmoja na kutafuta mkakati wa kutatua shida iliyopo. Tumekuwa tukifanya vizuri kwani mwaka 2018 tulikuwa watano kwa Mkoa wa Dar es Salaam na 40 kitaifa na tuko hapa Tabata Bonyokwa Segerea na hatuna tawi popote," alisema.

Mwalimu Mkuu huyo aliwashukuru walimu, wafanyakazi na mkurugenzi wa shule hiyo kwa ushirikiano waliotoa kuhakikisha shule hiyo inaendelea kupata mafanikio.

# Ndalichako aikunjulia kucha Suma JKT

INATOKA UK. 4

kwenye eneo zuri," alisema.

Prof. Ndalichako alisema majengo yanayotumiwa kwa sasa na wanafunzi ni hatarishi yanayoweza kuwaangukia wanafunzi kwa kuwa kuta zake zimepasuka kiasi cha kuona upande wa pili.

Alisema kwa uchunguzi wake wa awali, alibaini kuwa hakuna maelewano kati ya mkandarasi na mshauri elekezi ambaye ni BICO.

"Kinachoonekana hapa umejenga ghorofa mtoto, limejengwa hapa ili kuonyesha tu, lakini uhalisia hakuna kinachoendelea, hairidhishi kabisa," alisema.

Alitolea mfano wa ujezi wa Chuo cha Ualimu Kitangali ambacho kimejengwa na mkandarasi binafsi kwa gharama ya Sh. bilioni sita ambazo zilijenga nyumba za kisasa, ofisi na mabweni ambayo yana samani zote.

"Bico wafanye mapitio ya jengo kwa jengo hili tujue kwa nini eneo hili gharama ni kubwa zaidi wakati msimamizi wa ujenzi ni yule yule Bico ambaye alisimamia pa kajengwa kwa gharama za Sh. bilioni sita. Hatutaki maghorofa mtoto, tunataka majengo halisi vinginevyo tutachukua hatua za kisheria," alisema.

Awali, Kaimu Mkuu wa Kanda ya Ujenzi Suma JKT, Luteni Kanali Onesmo Njau, alisema ujenzi umekamilika kwa asilimia 30 na kwamba ukosefu wa vifaa vya

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
### PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
### MASASI TOWN COUNCIL

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MASASI TOWN COUNCIL

**STATEMENT OF FINANCIAL POSITION**
**AS AT 30 JUNE 2018**

| | Notes | 2018 TZS | 2017 TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash and cash equivalents | 23 | 1,747,878,170 | 1,222,997,270 |
| Receivables and prepayments | 24 | 170,344,196 | 362,582,189 |
| Inventories | 25 | 766,748,205 | 91,326,242 |
| Other financial assets | 0 | - | - |
| | | **2,684,970,570** | **1,676,905,700** |
| **Non-current assets** | | | |
| Other financial assets | 27 | 36,000,000 | 36,000,000 |
| Investments in associates | 0 | - | - |
| Property, plant and equipment | 26 | 17,651,926,636 | 18,496,678,054 |
| Intangible assets | 0 | - | - |
| Forestry assets | 0 | - | - |
| Investment property | 0 | - | - |
| | | **17,687,926,636** | **18,532,678,054** |
| Non-current assets held for sale | 0 | - | - |
| **TOTAL ASSETS** | | **20,372,897,206** | **20,209,583,754** |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current liabilities** | 28 | 25,297,444 | 124,976,183 |
| Payables | 29 | - | - |
| Short-term borrowings | 30 | - | - |
| Long-term borrowings | 31 | 136,819,132 | 50,734,900 |
| Employee benefits | 30 | 151,500,000 | - |
| Provisions | 11 | 369,305,652 | 215,053,420 |
| Deferred income (Grant) | | **682,922,228** | **390,764,503** |
| **Non-current liabilities** | 30 | - | - |
| Long-term borrowings | 31 | - | - |
| Employee benefits | 30 | - | - |
| Provisions(continget) | 29 | 19,513,091,613 | 19,504,621,904 |
| Deferred income (Grant) | | **19,513,091,613** | **19,504,621,904** |
| | | 20,196,013,841 | 19,895,386,407 |
| **TOTAL LIABILITIES** | | **176,883,365** | **314,197,347** |
| **NET ASSETS** | | | |
| **NET ASSETS** | | 176,883,365 | 314,197,347 |
| Accumulated surplus/(deficit) | | - | - |
| Revaluation surplus | | **176,883,365** | **314,197,347** |
| **TOTAL NET ASSETS** | | | |

The financial statements were authorised for issue by the Full Council on _26 th September 2018 and were signed on its behalf by:

Name: [illegible] Title: CHAIRMAN MASASI TC Signature: ____
Name: [illegible] Title: TOWN DIRECTOR Signature: ____

MWENYEKITI HALMASHAURI YA MJI MASASI
TOWN DIRECTOR MASASI TOWN COUNCIL P. O. BOX 447 MASASI

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MASASI TOWN COUNCIL

**STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE**
**FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2018**

| | Notes | 2018 TZS | 2017 TZS |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Local taxes | 9 | 812,546,063 | 868,096,872 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 404,622,905 | 392,375,993 |
| Amortisation of recurrent grants | 11 | 13,221,653,916 | 13,705,165,286 |
| Transfer from other Government entities | 12 | 91,241,675 | 331,100,465 |
| Revenue from exchange transactions | 13 | - | 26,619,000 |
| Finance income | - | - | - |
| Gain on foreign currency translation | - | - | - |
| Amortisation of capital grant | 29 | 454,966,428 | 535,717,788 |
| Other own source revenue | 14 | 760,365,949 | 817,706,043 |
| | | **15,745,396,936** | **16,676,781,448** |
| **Expenses** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 15 | 11,850,618,314 | 12,438,648,989 |
| Supplies and consumables used | 16 | 1,503,760,541 | 1,414,445,028 |
| Maintenance expenses | 17 | 54,180,199 | 698,985,486 |
| Grants and other transfer payments | 18 | 1,817,765,194 | 1,766,274,476 |
| Finance costs | 19 | 40,000 | - |
| Loss on foreign currency translation | 20 | - | - |
| Depreciation of property, plant and equipment | 26 | 505,453,786 | 573,787,173 |
| Impairment of property plant and equipment | 26 | - | - |
| Amortisation of intangible assets | 0 | - | - |
| | | **15,731,818,033** | **16,892,141,152** |
| Share of associates surplus/(deficit) | | - | - |
| **Surplus/(deficit) during the year** | | 13,578,903 | (215,359,705) |

The financial statements were authorised for issue by the Full Council on _26 th September 2018 and were signed on its behalf by:

Name: [illegible] Title: CHAIRMAN MASASI TC Signature: ____
Name: [illegible] Title: TOWN DIRECTOR Signature: ____

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MASASI TOWN COUNCIL

**CASH FLOW STATEMENT**
**FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2018**

| | Note | 2018 TZS | 2017 TZS |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| **Receipts** | | | |
| Local taxes | 9 | 801,760,552 | 868,096,872 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 404,622,905 | 392,375,993 |
| Receipt of revenue grants | 11 | 1,861,729,029 | 1,616,164,434 |
| Development Grants Received | 12 | 2,002,790,294 | 1,660,855,111 |
| Revenue from exchange transactions | 13 | - | 26,619,000 |
| Other own source revenue | 14 | 760,365,949 | 817,706,043 |
| **Payments** | | | |
| Employee costs | 15 | (970,048,545) | (1,355,913,742) |
| Payments to suppliers | 16 | (1,412,518,866) | (985,368,381) |
| Maintenance expenses | 17 | (54,180,199) | (698,985,486) |
| Grants and other transfer payments | 18 | (1,183,327,735) | (941,255,931) |
| Finance cost | 19 | (40,000) | - |
| **Net cash from operating activities** | | **2,211,153,384** | **1,400,293,912** |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Purchase of property, plant and equipment | | (1,686,272,488) | (896,966,401) |
| Investments with LGLB | | - | (9,000,000) |
| Purchase of intangible assets | | - | - |
| Purchase of investment property | | - | - |
| Acquisition of investments | | - | - |
| **Net cash from investing activities** | | **(1,686,272,488)** | **(905,966,401)** |
| **Cash flows from financing activities** | | | |
| Proceeds from borrowings | | - | - |
| Repayment of borrowings | | - | - |
| Development Grants Received | | - | 10,579,349 |
| Grants refunded/transferred | | - | **10,579,349** |
| **Net cash used in financing activities** | | | |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | | **524,880,899** | **504,906,863** |
| Cash and cash equivalents at beginning of period | | 1,222,997,270 | 718,090,408 |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | 24 | **1,747,878,170** | **1,222,997,270** |

The statement were authorised for issue by the Full Council held on 26 September, 2018 at the Council's Hall and signed by:

Name: [illegible] Title: CHAIRMAN MASASI TC Signature: ____
Name: [illegible] Title: TOWN DIRECTOR Signature: ____

**2.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL**

**To:** Hon. Chairperson of the Council,
Masasi Town Council,
P. O. Box 447,
**MASASI.**

**Re: Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statements of Masasi Town Council for the Financial Year ended 30th June, 2018**

**Unqualified Opinion**
I have audited the accompanying financial statements of Masasi Town Council, which comprise the statement of financial position as at 30th June 2018, statement of financial performance, cash flow statement, statement of changes in net assets/equity, and the statement of comparison of budget and actual amounts for the year then ended, as well as the notes to the financial statements, including a summary of significant accounting policies set out from page *8*.

In my opinion, the accompanying financial statements present fairly in all material respects, the financial position of Masasi Town Council as at 30th June, 2018, and its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) accrual basis of accounting and in the manner required by the Local Government Finances Act of 1982, revised 2000.

**Basis for Opinion**
I conducted my audit in accordance with International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under the said standards are further described in the Auditor's Responsibilities for the Audit of the financial statements section of my report. I am independent of Masasi Town Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the ethical requirements that are relevant to my audit of the financial statements in Tanzania, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements and the IESBA Code.

**Report on Other Legal and Regulatory Requirements**

**Compliance with the Public Procurement Act, 2011**
In view of my responsibility on the procurement legislation and taking into consideration the procurement transactions and processes I have reviewed as part of this audit, I state that, Masasi Town Council procurement transactions and processes have generally complied with the requirements of the Public Procurement Act No.7 of 2011 and its underlying Regulations of 2013.

Prof. Mussa Juma Assad,
Controller and Auditor General of the United Republic of Tanzania
March, 2019

National Audit Office of Tanzania,
Audit House,
4 Ukaguzi Road,
P.O. Box 950,
**41104 TAMBUKARELI,**
**DODOMA, TANZANIA.**
Tel: + 255 (022) 2321759
Fax: 255 (022) 2117527
Email: ocag@nao.go.tz

**Copy to;** Chief Secretary,
State House,
P. O. Box 9120,
1 Barack Obama Road,
**11400 DAR ES SALAAM.**

# Mawakala Tigo Pesa wanyakua kitita mil. 10/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu ya Tigo imetoa zawadi ya Sh. milioni 10 kwa washindi watatu wa promosheni ya tatu ya mawakala wa Tigo Pesa ikiwa ni sehemu ya kurudisha shukrani kwa mawakala wao nchi nzima.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi zawadi kwa washindi hao jana, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Tigo Pesa, Angelica Pesha, alisema promosheni hiyo ni kwa ajili ya kutoa shukrani kwa zaidi ya mawakala 100,000.

"Kwanza niwashukuru na kuwapongeza sana mawakala wetu wote kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhudumia wateja nchi nzima. Pili niwapongeze mawakala hawa watatu kwa kuibuka na ushindi kwa kuwapiku maelfu ya mawakala kweye mikoa yao," alisema

Huduma ya Tigo Pesa, alisema imekuwa zaidi ya mfumo wa kutuma na kupokea pesa bali ni sehemu ya shughuli zilizoanzishwa katika kuhakikisha inachangia agenda ya ujumuishwaji wa watu kiuchumi hasa katika kuwawezesha mawakala hao.

"Kama kampuni ya kidigitali tunahakikisha tunakuja na mikakati mbalimbali ambayo itawafanya mawakala nchi nzima kunufaika na huduma hii.

"Tuna furaha kuchangia agenda ya ujumuishaji wa watu kiuchumi kupitia huduma ya Tigo Pesa kwa kurahisisha huduma za kifedha jambo linalochochea ukuaji wa uchumi kwa mawakala, jamii na nchi kwa ujumla," alisema Pesha.

Pesha aliwataja washindi hao kuwa ni Suleiman Hussein kutoka Zanzibar aliyeshinda Sh. Milioni tano, Vicky Ibrahim wa Temeke aliyeibuka na Sh. Milioni tatu na Anna Mosha kutoka Ilala aliyejishindia Sh. milioni mbili.

Promosheni hiyo ijulikanayo kama 'Tigo Pesa Wakala promosheni' ilianza Septemba, mwaka huu na washindi 12 wametoka katika kanda nne za Tigo ambazo ni Kanda ya Ziwa, Pwani, Nyanda za Juu Kusini na Kaskazini.

# RC aagiza wawekezaji waswekwe ndani

**Na Allan Isack,** KITETO

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amemwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Kiteto, Fadhil Luoga, kuwakamata wachimbaji wa madini ya Ruby katika Kijiji cha Orkine wanaofanya utafiti wa madini hayo kinyume cha sheria.

Mnyeti alitoa agizo hilo juzi baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa Orkine ya kutokupata msaada wowote kutoka kwa wachimbaji hao ambao kila mwaka wanadai wanafanya utafiti.

Alisema Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Tumaini Magessa, alishaagiza wasimamishe kufanya kazi katika eneo hilo, kutokana na kufanya utafiti kwa kipindi cha miaka 20 bila kuonekana kwa faida yoyote.

Mkuu wa mkoa alisema si sahihi wachimbaji hao kufanya utafiti zaidi ya miaka 20 kwa kuwa wanapaswa kutafiti kwa miaka minne na wakiona kuna madini wakate leseni kwenye Tume ya Madini halafu wazungumze na wanakijiji. "Kama wana leseni ya utafiti huwa haizidi miaka minne, watuambie kama kuna madini au hakuna na kama hayapo wanatakiwa kuondoka. Lakini endapo wamegundua kuna madini, wanapaswa kufuata utaratibu wa kukata leseni," alisema Mnyeti.

Alisema hata wangekuta kuna madini na kupata leseni wanapaswa kuwa na ushirikiano na kijiji na kulipa kodi ya huduma kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto.

"Nakuagiza OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) wakamate hawa watu wote waweke rumande waseme wanachimba kwa mamlaka gani kwa sababu wameshazuiwa kuchimba hawasikii na kwa nini wanaendelea kuchimba," alisema.

Kwa upande wake, Magessa alisema suala hilo alilifahamu mapema na alishamwagiza ofisa madini kufanya ukaguzi na ilibainika kuwa katika eneo hilo kuna madini lakini yapo chini ya kiwango.

Magessa alisema aliagiza shughuli hizo zisitishwe lakini alishangazwa kuambiwa kuwa bado wanaendelea na uchimbaji kwa kisingizio cha utafiti.

Mkazi wa kijiji hicho, Hassan Mkopi, alisema amesikitishwa na wachimbaji hao ambao kila siku wamekuwa wakidai wapo kwenye majaribio zaidi ya miaka 20 na inapotokea kijiji kinaomba msaada, hawasaidii kitu chochote.




Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro (katikati), akizindua utoaji wa chanjo ya Surua, Rubella na Polio, katika hospitali ya Levolosi, iliyopo jijini Arusha jana. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Vikundi 17 vyalamba mikopo ya mil. 50/-

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

OFISA Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Longido, Grace Mghase, amesema katika mwaka wa fedha 2019/20 wanatarajia kutoa Sh. million 150 kutoka katika mapato ya ndani kukopesha vikundi vya wanawake, vijana na walemavu.

Mghase alisema hayo juzi wakati wa kukabidhi hundi yenye thamani ya Sh. milioni 50 kwa vikundi 17 kutoka kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 .

Alisema vikundi hivyo vimesajiliwa na vinaratibiwa na idara ya maendeleo ya jamii, lengo likiwa kuwajengea uwezo wananchi katika wilaya hiyo ili kukabiliana na changamoto mbalimbali za kimaisha na kubuni njia za kuzalisha kipato tofauti na kutegemea ufugaji pekee.

Changamoto kubwa inayovikabili vikundi vingi, alisema ni utegemezi wa miradi ya ufugaji ambayo huathiriwa na ukame wa mara kwa mara.

Pia alitaja changamoto nyingine inayoikabili wanavikundi hao ni kutokujua kusoma na kuandika, hivyo husababisha kushindwa kutunza kumbukumbu za fedha kwa usahihi.

"Vikundi vilivyopewa mikopo ni 17, wanawake saba walipokea millioni 20, Vijana sita walichukua millioni 20, na walemavu wanne walipewa millioni 10, licha ya kupewa mikopo hiyo walipatiwa elimu ya ujasiriamali ikiwemo kutengeneza nguo aina ya batiki," alisema Grace.

Mbunge wa Longido, Dk. Steven Kiruswa, aliomba idara hiyo kuangalia uwezekano wa kutolewa kwa elimu ya watu wazima, tofauti na ya ujasiriamali ili kuwasaidia wale wasiojua kusoma na kuandika.

Akikabidhi hundi ya fedha kwa vikundi hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, aliwataka wanufaika wa fedha hizo kuzitumia kwa matumizi sahihi na kurejesha kwa wakati ili kutoa nafasi kwa vikundi vingine kukopeshwa.

Pia aliitaka halmashauri hiyo, kuhakikisha mikopo hiyo inafikia vikundi 18 vilivyoko katika kata za Longido na kuwataka kuacha tabia ya kurudia kutoa mikopo hiyo kwa kata moja mara kwa mara..

Mathayo Kunana, ambaye ni mlemavu kutoka kata ya Kitumbeine, aliishukuru serikali kwa kuyatambua makundi yenye ulemavu kwa kuweka mikakati ya kuyainua kiuchumi. Alisema miaka ya nyuma watu wenye ulemavu walionewa na hawakusaidiwa na pia walisahaulika kabisa ndani ya jamii.

# Watoto 87,332 kuchanjwa surua

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HOSPITALI za Wilaya ya Arusha zinatarajia kutoa huduma za chanjo ya polio na surua kwa watoto 87,332 wenye umri kuanzia miezi tisa hadi miaka mitano kwa muda wa siku tano kuanzia juzi. Akizungumza juzi jijini hapa wakati wa ufunguzi wa chanjo hiyo katika hospitali ya Levolosi, Mganga Mkuu wa Jiji la Arusha, Dk. Simon Chacha, alisema watoto 51,366 wanatarajia kupata chanjo ya surua na wengine 35,966 chanjo ya polio.

"Kwa upande wa wilaya hali ya uchanjaji imefikia asilimia 117 kwa sababu wanaopatiwa matibabu wengine wanatoka katika wilaya zingine, hivyo asilimia kubwa wanapatiwa huduma kwa Arusha mjini ndiyo maana huduma hii inaongezeka na tutaisambaza katika maeneo yote yenye wakazi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, alisema chanjo hizo ni muhimu kwa kuwa watoto wasipopatiwa itawasababishia ulemavu na baadaye kupoteza maisha, hivyo ni vyema wazazi wahakikishe watoto wao wanapata chanjo zote tisa ili kuepukana na magonjwa ya maambukizi na ulemavu.

Daqarro aliongeza kuwa ndani ya Wilaya ya Arusha, dawa zinapatikana kwa asilimia 95 hadi 98 na wananchi wa wilaya hiyo, wakae tayari kupata huduma kwenye hospital ya wilaya muda si mrefu.

"Hospitali hii itakamilika siku za karibuni, hivyo huduma zitaendelea kuwa imara na nawaomba wananchi mwendelee kuwa na umoja na serikali ili kufanikisha malengo yaliyopo," alisema. Katibu wa Lions Club Arusha, Maswanya Yusuf, alisema wadhamini wa chanjo hizo wataendelea kuhamasisha wananchi ili chanjo iwafikie watoto wote na lengo kubwa nikuwaepusha watoto na magonjwa ya kuambukizwa .

Mmoja wa wazazi wa watoto waliopatiwa chanjo hizo, Fatuma Khalidi, aliishukuru serikali na wadau wa afya kwa kuwapatia watoto wao chanjo hizo muhimu.

# Ataka udhibiti wa mlipuko magonjwa

**Na Mary Mosha,** SAME

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mhgwira, ameagiza hatua za haraka zichukuliwe kuzuia kujitokeza kwa magonjwa ya kipindupindu na kuhara katika Soko la Mwembe, wilayani hapa.

Pia ametaka Mkuu wa Wilaya hiyo, Rosemary Senyamule, kumwajibisha Ofisa Afya anayesimamia soko hilo kutokana na kuruhusu kufanyika biashara bila kuwapo huduma ya choo.

Dk. Mghwira alitoa maelekezo hayo juzi alipokwenda kusikiliza kero za wafanyabiashara wa soko hilo la Mwembe.

Akiwa katika soko hilo, Dk. Mghwira alisema kukosekana kwa huduma ya choo katika soko hilo kunatishia kuibuka tena kwa magonjwa ya mlipuko ya kipindupindu.

Kutokana na tishio hilo, alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Same hadi kufikia Novemba, mwaka huu, ahakikishe choo kipya kimejengwa katika soko hilo.

Baadhi ya wafanyabiashara wadogo wa soko hilo, walisema kuna umuhimu wa choo katika soko kwa kuwa kumekuwapo na magonjwa ya mlipuko ya kila mara hasa nyakati za mvua.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Edward Msofe, alisema wanalazimika kujisaidia pembezoni mwa kuta zilizoko katika soko hilo kutokana na kukosekana choo kwa muda mrefu .

"Kukosekana kwa choo katika soko hili kunatulazimisha kujisaidia vichakani hali ambayo ni hatari kwa afya zetu lakini hatuna namna. Tunaomba serikali ituangalie kwa namna ya pekee," alisema.

Akipokea maelekezo hayo, Senyamule alisema tayari wametenga eneo lingine kwa ajili ya kuhamishia soko hilo.

"Tumepokea maelekezo yako Mkuu wa Mkoa. Tutayafanyia kazi lakini tayari tumeshatenga eneo lingine kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa soko ambalo litakuwa na miundombinu rafiki kwa wafanyabiashara," alisema.

# Kampeni ya surua yaanza kwa kasi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KAMPENI ya chanjo ya surua, rubella na polio imeanza rasmi kutolewa kwa kasi ya aina yake katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, baada ya idara ya afya kueleza kuwa walengwa watakaofikiwa ni zaidi ya watoto 44,000.

Utaratibu huo hufanyika kila baada ya miaka mitatu ili kupunguza kwa kiasi kikubwa kama siyo kutokomeza kabisa magonjwa ya surua, rubella na polio ambayo yanapopuuzwa husababisha ulemavu wa kudumu na hata vifo kwa waathirika.

Mratibu wa Chanjo wa Wilaya ya Hai, Michael Ndowa, aliyasema hayo jana wakati Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, alipokwenda katika hospitali ya wilaya kuzindua kampeni hiyo.

Kampeni hiyo itatekelezwa kwa siku tano kuanzia Oktoba 17 hadi 21 mwaka huu.

Sera ya Afya ya Mwaka 1990 ina lengo la kuinua hali ya afya kwa wananchi wote mahali popote walipo ikiwa ni mijini au vijijini kwa kupunguza maradhi na vifo kwa wananchi na kuongeza umri wa maisha yao kwa kuwa na afya thabiti kimwili, kiakili na kijamii.

"Maandalizi yote yamekamilika na zoezi linaanza rasmi leo (jana) katika sehemu mbali mbali za wilaya yetu. Lengo la Wizara ya Afya ni kuhakikisha watoto wote wanapata chanjo hii ya Surua, Rubella na Polio ili kukabiliana na magonjwa yanayosababishwa na kutokupata chanjo hizo.

"Na kimsingi, tunatarajia kwamba zaidi ya watoto 28,000 wenye umri kuanzia miezi tisa hadi miaka minne na miezi 11, watapatiwa chanjo ya surua na rubella. Lakini pia zaidi ya watoto 16,000 wenye umri wa mwaka mmoja na nusu hadi miaka mitatu na nusu watapatiwa chanjo ya polio," alisema.

Akizindua kampeni hiyo, Ole Sabaya aliwataka watumishi wote wa umma katika wilaya hiyo kushirikiana na idara ya afya kuhamasisha wazazi na walezi wenye watoto, kuhakikisha kila mtoto wenye umri unaostahili kupewa chanjo hiyo, anapatiwa chanjo stahiki.

"Serikali imegharamia gharama zote za chanjo hii na ndio maana inatolewa bure kwa watoto. Hatuwezi kupoteza mtoto kwa kupooza kwa kukosa chanjo, hivyo ninyi wazazi na walezi mliofika hapa hospitali ya wilaya, mhamasishe wengine wote washiriki kikamilifu katika zoezi hili,"alisisitiza Ole Sabaya

Ugonjwa wa rubbela ambao dalili zake zinashabihiana kwa karibu na surua, ugonjwa huu husababishwa na virus vya rubella na huenezwa kwa njia ya hewa, ingawa pia hata mjamzito huweza kumuambukiza mtoto tumboni kwa njia hiyo. Ugonjwa huu kama surua, pia huweza kuwapata watu wazima ingawa watoto ndio zaidi.

Dalili zake pia ni pamoja na vipele vidogo vidogo kwenye ngozi, homa na macho kuwa mekundu. Nyingine ni uchovu wa mwili, vidonda kooni, uvimbe kwenye matezi na mafua.

Aidha, ugonjwa wa polio nao huambukizwa na virusi vijulikanavyo kitaalamu kama polio virus na huweza kumpata mtu wa umri wowote, lakini hasa zaidi watoto walio chini ya umri wa miaka 15.

Surua kwa mujibu wa wataalamu wa afya, ni ugonjwa unaosababishwa na virusi aina ya 'morbillivurus paramyxvirus' vinavyoenea kwa haraka. Ugonjwa huu huathiri watu wa rika zote lakini zaidi ni watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.




Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, akisoma mabango yenye kero mbalimbali za wananchi wa Kijiji cha Namelock, wilayani Kiteto, alipofanya ziara kijijini hapo, jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Walalamikia kutozwa michango bila sababu

**Na Mary Mosha,** SAME

WAKAZI wa Kata ya Hedaru, Same mkoani Kilimanjaro, wamepeleka malalamiko yao kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mhgwira, juu ya michango ya Sh. 250 kwa kila mwananchi bila kujua fedha hizo zinatumikaje.

Waliowasilisha malalamiko hayo ni wananchi wa Kitongoji cha Gundu Sinde ambao kwa umoja wao wanadai kwamba viongozi wa kitongoji hicho wanatoa sababu ambazo haziwaridhishi.

Akiwasilisha malalamiko hayo kwa niaba ya wenzake, Restina Ahadia, alisema kila mwezi wamekuwa wakichangishwa Sh. 250 kwa madai ya kulipia mshahara wa mlinzi, ingawa wanajua analipwa na serikali.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, tunaomba kauli yako ili tujue kama ni halali sisi kuchanga fedha za mshahara wa mlinzi kwa mujibu wa taratibu za serikali au laa," alisema Ahadia

Mwananchi huyo alisema viongozi hao wa vitongoji wamekuwa wakichangisha fedha hizo bila kuzitolea ufafanuzi huku wakitishwa kunyimwa huduma za kijamii endapo watakaidi kulipa fedha hiyo.

Akijibu malalamiko hayo, Dk. Mghwira alisema utaratibu huo haupo kwenye serikali na amechukua malalamiko hayo kama changamoto na atayapatia ufumbuzi haraka iwezekanavyo.

Aidha, Mghwira aliitaka halmashauri ya wilaya ya hiyo, kuhakikisha inafanya ukarabati wa soko la Hedaru ili kuwasaidia wafanyabiashara hao kufanya shughuli zao katika mazingira rafiki.

"Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya (Anna Claire Shija), hakikisha miundombinu ya soko hili inaboreshwa. Wafanyabiashara wamelalamikia miundombinu ya soko, usafi wa vyoo, kutokuwapo kwa umeme katika soko na vijiji jirani licha ya kuwapo kwa umeme wa REA (Wakala wa Nishati Vijijini)," alisema.

Kuhusu barabara, mkuu huyo aliizitaka mamlaka husika kuhakikisha inashughulikia barabara zote za vijijini zinazowasaidia wakulima kupeleka mazao yao sokoni.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Hedaru, Jackson Mbwambo, alisema amepokea changamoto zote na zitafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria.





Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi (kushoto), akiimba wimbo kwa kurukaruka na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Mtanana, wilayani humo, mkoani Dodoma, alipotembelea kukagua miradi ya elimu shuleni hapo, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watakiwa kujiunga na elimu ya ufundi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIJANA wanaohitimu elimu ya msingi na sekondari wametakiwa kujiunga na vyuo vya ufundi ili kujikwamua kiuchumi badala ya kukaa vijiweni na kujiingiza kwenye makundi ya uhalifu. Wito huo ulitolewa jana na wahitimu wa mafunzo ya ushonaji wa Chuo cha ushonaji cha Tailoring Beach Center Dodoma wakati wa mahafali yao, yaliyofanyika jijini hapa.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu hao, Joyce Daud, alisema vijana hawana sababu ya kukaa vijiweni na kuinyooshea serikali vidole kwa kukosa ajira wakati zipo fursa nyingi za kuwawezesha kujikwamua kiuchumi kupitia mafunzo ya ufundi.

Alisema kitendo cha kukaa vijiweni kinasababisha kujihusisha na uhalifu. Kwa upande wake, Mkuu wa chuo hicho, Richard Mnemele, aliwataka wazazi na walezi kuwaendeleza vijana wao kielimu kupitia mafunzo ya ufundi ili kushiriki kwenye kuifikia azma ya serikali ya kufikia uchumi wa kati na wa viwanda. "Msiwaachie kuzunguka mitaani na kukaa vijiweni wapelekeni vyuo vya ufundi wapate ujuzi utakaowasaidia kuajiriwa na kuajiri wengine,"alisisitiza.

Vile vile Mkuu wa Chuo alisema changamoto iliyopo kwa wazazi na walezi zama hizi ni kuwa na mtazamo kuwa kijana anapohitimu elimu hiyo anapaswa kutafutiwa kazi bila kutambua umuhimu wa elimu ya ufundi.

Naye, Mussa Kawea, mhitimu, aliwataka waliomaliza mafunzo hayo kutumia fursa waliyoipata kujiinua kiuchumi kwenye kaya zao na kuwa na viwanda vya ushonaji.

# Jamii yaonywa kuchezea surua

**Na Renatha Msungu,** BAHI

WAKAZI wa Wilaya ya Bahi wametakiwa kuacha kuwatibu kienyeji watoto wenye ugonjwa wa surua badala yake wapelekwe vituo vya kutolea huduma za afya ili kupata tiba sahihi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, Dk.Best Magoma, baada ya mkazi wa Bahi, Angelina Hamis, kueleza kuwa alilazimika kumficha mtoto wake ndani na kumtibu kienyeji alipopata ugonjwa wa surua.

Akizungumza katika uzinduzi wa chanjo ya surua rubella na polio, mama huyo alisema aliamua kufanya hivyo kwa kuwa aliambiwa akipelekwa hospitali akichomwa sindano ugonjwa huo utahamia tumboni.

"Mtoto wangu alipata dalili za ugonjwa huo mama mmoja akaniambia nimfiche ndani baada ya siku mbili niliona hali ya mtoto inazidi kuwa mbaya nikatoroka kumpeleka hospitali na tulifanikiwa kupata matibabu na mwanangu alipona," alisema Angelina.

Alieleza kuwa elimu kuhusu ugonjwa huo inahitajika hasa kwa wakazi wa vijijini ambao wanaamini surua inatibika kienyeji.

Kufuatia simulizi hiyo, Dk.Magoma alisema hakuna sababu ya kuwaficha ndani watoto kwa kuwa ugonjwa huo unatibika hospitalini na pia una chanjo.

"Hizi ni imani potofu kinachotakiwa kwa sasa ni kuwapeleka watoto wenye umri chini ya miaka mitano kupata chanjo za surua, rubella na polio ili kuzuia kupata magonjwa hayo,"alisema Mganga Mkuu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi, Mganga Mkuu Hospitali ya Wilaya ya Bahi Dk. Philipina Philipo, aliwasisitiza wananchi wa eneo hilo kutumia siku tano za kampeni ya utoaji chanjo kupeleka watoto kwenye vituo vya afya ili kupata huduma.

Alisema wilaya hiyo imejipanga kutoa chanjo kwa watoto 44,035 kwenye magonjwa hayo na watoto wengine 19,667 wao watapatiwa chanjo ya polio.

Akizindua utoaji chanjo, Mkuu wa Wilaya ya Bahi Mwanahamisi Munkunda, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk.Binilith Mahenge, aliwataka wananchi kupeleka watoto kwenye vituo hivyo ili waweze kupata chanjo.

Alisema kazi ya utoaji chanjo ina umuhimu mkubwa kwani ni njia ya kuwaokoa kwa kuwaepusha watoto na vifo vitokanavyo na magonjwa hayo.

# 96,000 kuchanjwa wilayani Dodoma

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATOTO 96,336 wa Wilaya ya Dodoma wanaendelea kupatiwa chanjo za polio, surua na rubella ili kuwalinda na kuwaepisha na magonjwa hayo yanayosababisha ulemavu na vifo.

Hayo yalisemwa jana na Mratibu wa Chanjo Jiji la Dodoma Consolata Urio, àlipokuwa akizungumza na wanahabari akihamasisha kampeni ya utoaji chanjo ambayo itafanyika kwa siku tano, ilianza juzi.

Alisema kuwa kati ya idadi hiyo ya watoto 61,500 watachanjwa surua na rubella na wengine 34,836 watachanjwa polio.

Alieleza kuwa chanjo hiyo itatolewa na wataalum wa afya kwenye vituo vya afya 60 ambavyo vitakuwa vya muda na kuhamahama.


"Chanjo hii itakuwa ya siku tano kuanzia Oktoba 17- 21 mwaka huu, wahudumu mbali na kutoa huduma kwenye vituo vya afya pia watawafikia kuwahudumia watoto kwenye shule, ,minadani na vituo vya mabasi,"alisema Mratibu huyo

Aliwataka wazazi na walezi kuwapeleka watoto kwenye vituo vya afya ili kupata chanjo na kuwaepusha na kuwakinga na magonjwa hayo.

Aidha, aliwataka wazazi na walezi kuacha imani potofu juu ya chanjo zinazotolewa kwa watoto hao kwani ni salama na hazina madhara yoyote.

Alieleza kuwa kumekuwepo na mtazamo kuwa mtoto akipata chanjo atapata ulemavu jambo ambalo si kweli.

Mratibu huyo alisema chanjo hiyo inatolewa bure kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya na watawafikia watoto wote na waliopo vijijini na maeneo mengine kwa kutumia vituo vya kuhamahama.





Baadhi ya wananchi wakiwa na mbwa wao, katika mji wa Kiomboi, wilayani Iramba, wakiwa wamejitokeza kwenye moja ya kituo cha ofisi ya idara ya mifugo na uvuvi, kwa ajili ya chanjo ya mbwa na paka iliyoendeshwa wilayani humo mkoani Singida jana, kupitia ufadhili wa shirika linalojihusisha na wanyama la EAAW. **PICHA: ELISANTE JOHN**

# Anaswa kuagiza dawa kinyemela

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (Zaeca), inamshikilia raia wa India, Nootan Ramaiya (54), kwa tuhuma za kuagiza dawa za binadamu bila kufuata taratibu na sheria.

Mtuhumiwa huyo anahojiwa baada ya kubainika kuwa ameingiza zaidi ya kilo 100 za dawa za binadamu, bila kufuata utaratibu na sheria zinazotakiwa.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana mjini hapa, Kaimu Mkurugenzi wa Uchunguzi na Operesheni wa Zaeca, Makame Khamis Hassan, alisema Ramaiya alikamatwa kwenye uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Aman Karume , akitokea nchini India akiwa na mabegi kadhaa yaliyobeba dawa hizo.

Alieleza kuwa rai huyo wa India tayari amefanyiwa mahojiano ili taratibu za kiuchunguzi ziweze kuendelea na mara baada ya kukamilika, jalada litapelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Dawa na Vipodozi wa Wakala wa Chakula na Dawa Zanzibar, Nasssir Buhet, alisema dawa hizo ni sahihi kwa matumizi ya binadamu lakini zimeingizwa kinyume na utaratibu wa sheria za Zanzibar.

Katika mazungumzo hayo alitoa wito kwa wafanyabiashara kufuata taratibu katika uingizaji wa bidhaa zao kutoka nje ili kuepuka usumbufu usio wa lazima na hata wakati mwingine kupambana na mkono wa dola.

# Vijana watambia teknolojia mpya

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Mamlaka ya Amali Zanzibar, Bakari Ali Silima, amewataka vijana kutumia teknolojia mpya ya mawasiliano ya 'internet thing' kwa ukamilifu ili kukusanya taarifa mbalimbali za kijamii na pia kujiajiri.

Akizungumza na vijana kwenye mkutano uliofanyika Vuga, wakati akifungua mafunzo ya matumizi ya teknolojia hiyo ya 'internet thing', aliwataka vijana hao kuona kuwa wanafaidika na mafunzo hayo na teknolojia pia.

Aliwaambia kuwa watazidi kunufaika na teknolojia hiyo kwani itazidi kukuza elimu katika vyuo vikuu kwa kuwezesha kusoma vitabu na majarida mbalimbali kieletroniki na kwa urahisi.

Aidha, wataweza pia kufanya shughuli nyingine za kijamii kama kujifunza utaalam wa kilimo na uvuvi.

Vilevile, alisema teknolojia hiyo ina fursa nyingi kama vile kuwawezesha kutumia simu za mkononi, kwani itawarahisishia kupata mitandao mingine ya kijamii .

Aliwaambia kuwa manufaa mengine ni kupata mbinu mbalimbali za kujiajiri wenyewe na kuwawezesha kufanya mambo mengi na bora zaidi.

Alisema wanaweza kurahisisha kufanya shughuli kama uvuvi kwa upande wa baharini na kwa nchi kavu wataitumia kwenye kilimo bila ya kwenda shambani na pia inaweza kutumika kama CCTV kwa ulinzi wa mali na kuimarisha usalama nyumbani.

Hivyo aliwahimiza vijana kuitumia fursa hiyo ambayo inaweza kuwapatia ajira na kujiendeleza kimaisha na pia kujiongezea utaalamu na kipato.

Naye Mkuu wa Shule ya Elimu Endelezi na Utaalamu inayohusiana na Teknolojia ya internet thing , Dk. Haji Ali Haji, alisema taaluma hiyo ni mpya kwa Zanzibar ambayo inalenga jitihada za kukuza teknolojia na kuwataka kuyazingatia mafunzo hayo wanayopatiwa ili wakimaliza wayafanyie kazi.

Aidha, alisema teknolojia hiyo inarahisisha mambo mengi ikiwamo kutumia simu ya mkononi kwa kuingiza kila unachotaka , kufanya utafiti, mazingira na hata mambo ya utalii.

Kwa upande wa mtaalamu wa mafunzo hayo kutoka Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Copenhagen, nchini Denmark, Sebastian, teknolojia hiyo ni muhimu kwa vijana.

Aliwataka waitumie kikamilifu kwani itawarahisishia mambo mengi hasa kwa kutumia simu za mkononi.

Mafunzo ya kozi hiyo ya muda yamewashirikisha vijana kutoka vyuo vikuu mbali mbali vya Zanzibar ambao wameahidi kuyafanyia kazi.

# 'Msitegemee vivuli vya viongozi'

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAFANYAKAZI wa Wizara ya Ardhi, Maji, Nyumba na Nishati , kisiwani Pemba, wametakiwa kuacha kufanya kazi kwa kutumia vivuli vya viongozi.

Aidha, wameonywa kuacha kufanyakazi kwa mazoea badala yake wafuate sheria na kanuni za utumishi wa umma katika utendaji wao.

Hayo yalielezwa na Ofisa Mdhamini Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Massoud Ali Mohammed, alipokuwa akifungua mkutano ulioandaliwa na Ofisi ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, uliofanyika Gombani.

Mafunzo hayo yalilenga kuzungumzia umuhimu wa maadili ya viongozi kwa watumishi wa umma.

Alionya kuwa mtumishi yeyote analindwa na sheria na kanuni za utumishi, hivyo ni vyema pale zinapotokea kasoro kwa watendaji na viongozi wao kufuata utaratibu jambo ambalo litaongeza ufanisi katika utendaji wa kila siku wa kazi ndani ya taasisi zenyewe kwa taifa.

Alisema ni vyema kila mfanyakazi wa umma kuelewa na kufuata maadili ya kazi zao ili kuondosha migogoro inayojitokeza baina ya watu wanaowahudumia na kuepusha chuki zisizo za lazima.

Aidha, Ofisa Mdhamini aliwataka watumishi hao kuwa na uelewa wa kujua maadili ya viongozi wa umma badala ya kuiachia tume pekee kushughulikia suala hilo kwani watumishi na jamii inahusika katika kutoa taarifa za ukiukwaji wa maadili.

Akitoa maelezo kwa watumishi hao Msaidizi Mkuu Idara ya Usajili Kumbukumbu na Uhakiki Tume ya Maadili ya Viongozi Pemba, Suhaila Mohammed Iddi, alisema kiongozi hatakiwi kujihusisha na migongano ya maslahi ya umma bali afuate utaratibu katika kufanya kazi zake ili jamii imuelewe kwa maslahi yao na ya taifa.

Akielezea baadhi ya athari ya maadili ya kiongozi katika taasisi kukiuka maadili, Ofisa Uhusiano na Elimu Tume ya Maadili Zanzibar Haji Juma Chapa, alisema endapo kiongozi atakiuka maadili wachache ndio wataofaidika.

Aidha hali hiyo itapelekea kuporomoka kwa utendaji wa kazi sambamba na kuiongezea mzigo serikali kwa kuonekana kuwa haiko imara kiuongozi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT



**BEYONCE AWAUMIZA WATU KWA UREMBO** Soma UK.20

JUMAMOSI OKTOBA 19 2019



**WANAPIGA PESA**

# Kupitia ustaa, urembo wao

## BASI SAWA



## Amini umetoa nyongo, sasa tulia

MWANAMUZIKI Amini amesema tasnia ya muziki imetawaliwa na fitina na unafiki kutokana na baadhi ya watu kuwashusha watu wasiowapenda.

Amesema kwa msanii ambaye anafanya kazi peke yake si rahisi kufika mbali kutokana na hali mbaya iliyokuwepo kwa sasa.

"Mimi napambana na hali hiyo najifananisha na maji ambayo yanaweza kupita hata katika ukuta wa zege, siogopi hali hiyo lakini ukweli hali ni mbaya kutokana na watu kuamua kuwashusha wasiowapenda na kuwapandisha wale wanaonufaika nao," alisema Amini.



## Nyerere kama kweli basi wewe mzalendo

MSANII wa filamu, Steve Nyerere, amesema kupitia umoja wao wa Uzalendo Kwanza, wana mpango wa kujenga wodi ya wazazi katika hospitali ya Vijibweni jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati akikabidhi vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni tano, amesema jengo hilo likikamilika litaitwa Uzalendo Kwanza kama njia ya kuunga mkono juhudi ya rais Dk. John Magubuli.

"Sisi kama asasi ya wasanii tumeona tuna jukumu la kuunga mkono serikali yetu kwa kujenga wodi ya mama na mtoto katika hospitali hii, kazi hiyo itaanza hivi karibuni," amesema Steve Nyerere.



# Dogo Janja awehuka na mapenzi Harua

MKALI wa muziki Dogo janja, amesema ana mpango wa kutangaza ndoa ili kuepukana na vitendo vya zinaa vinavyomkasirisha Mungu.

Amesema kwa sasa anajiona amebadilika kitabia kutokana na kuwa na mwanamke mwenye upeo na hofu ya Mungu na mnyenyekevu kwa mwanamume.

Pia amempiga dongo la kiaina mke wake wa zamani Irene Uwoya, kwa kueleza huyu wa sasa hana tabia ya kupenda mitandao na kujianika ovyo kama hana mwanaume.

Uwoya amekuwa mpenzi wa mitandao ya kijamii kiasi kila siku haiwezi kupita bila kuposti kitu ambacho wakati mwingine kinaibua mjadala mkali kwa wafuasi wake.

"Najiona mwenye furaha zaidi kumpata mwanamke mwenye hofu ya mungu na ambaye amejitahidi kubadilisha mwenendo wangu kiasi kikubwa. Nashukuru huyu hana mapenzi na mitandao ya kijamii hapendi kujianika ovyo," amesema Dogo Janja.

## INSTA-TWITTER





**Kaka** yangu Haji Manara kinachokubakiza Kigali, Rwanda mpaka sasa hivi ni nini aisee? Au watu wazima tujiongeze? Maana Iringa unakaaga siku moja tu ya pili unataka kurudi, ila sasa Rwanda inakata wiki, vipi aisee?!!!-**MC Pilipili.**



**Kwa** sisi tuliokua kwenye hali mbaya hatuna kitu, lakini tulikuwa na upendo sana, karne hii upendo hakuna kabisa-**Ally Choki.**



# Vanessa 'Bado' utamu ule ule

SINGO mpya ya mwanamuziki Vanessa Mdee akimshirikisha Rayvanny imezidi kupaa siku nne baada ya kuachiwa video yake mtandaoni.

Kulingana na mtandao wa You tube, wimbo huo unaoitwa 'Bado' umeshafikisha wazamaji 300,000 huku ukiongoza kuwa na mvuto wa kipekee zaidi.Baadhi ya watu waliotoa maoni yao wamsema, video hiyo inaonyesha jinsi gani mwanamuziki huyo anavyoonesha kipaji chake cha hali ya juu katika fani hiyo.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

## UNASEMAAA...

# Kala atoa ushauri kwa wanaojirekodi

RAPA Kala Jeremiah ametoa ushauri kwa watu wanaotumia simu za mikononi kujirekodi kuachana na tabia hiyo kwani kuna hatari ya kudukuliwa na watu wabaya.

Akizungumzia sakata la msanii mwenzake Menina ambaye video zake za faragha zimesambaa mitandaoni, amesema jambo hilo hafurahishwi nalo hata kidogo kwani limevuka mipaka ya utu.

"Nawaomba watu wasijirekodi na simu, simu hazina siri kila mtu anaweza kuzidukua bora hata mjiangalie kwenye kioo au mjirekodi na kamera ya kawaida," amesema Kala.




## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Kuanzisha** kila kitu ni ngumu. Kuanzisha biashara ngumu, mapenzi ni magumu, kufanya mazoezi ngumu, kuzeeka ngumu, kufa ndiyo kabisa. Ugumu ndiyo rangi ya maisha-**Nikki wa Pilli.**



**Tarehe** 14 Oktoba nilitimiza miaka mitatu kwenye ndoa yangu. Dhumuni la kuoa Nyerere Day nitawaambia hivi karibuni-**Tunda Man.**



**Kila** asubuhi swala huamka akijua kuwa lazima awe na kasi zaidi kuliko simba mwenye kasi ili asiliwe. Simba pia huamka akijua lazima awe na kasi kuliko swala ili asilale njaa. Bila kujali wewe ni swala au simba, jua likichomoza ni bora uanze kukimbia kwa kasi-**Steve Nyerere.**

# Kuumbe!



SANAA SI UADUI

## Bongofleva jifunzeni Nigeria

KWA wanamuziki wa Bongo ni jambo lisilozoeleka kuwaona wasanii wakinunuliana zawadi kwa ajili ya kupongezana au kuimarisha fani yao.

Kila kukicha kwenye mitandao ya kijamii utakuta wasanii wa Bongo fleva wakilumbana na wengine wakisemeana ovyo kana kwamba sanaa hiyo imekuwa uadui.

Huwezi kusikia mmoja anatangaza kumkubali mwenzake kutokana na kazi yake kuwa nzuri. Badala yake utawasikia wakitoana kasoro na majigambo yasiyo na maana.

Lakini huko Nigeria mambo ni tofauti kwani huko msanii mmoja kumsifia mwingine ni jambo la kawaida sana, tena wakati mwingine wanapeana zawadi zenye gharama kubwa kama ishara ya kumkubali.

Ndivyo mkali wa muziki kutoka nchini humo, Davido, alipoamua kununua mkufu wa gharama kwa ajili ya kumtunza mwanamuziki wake kuonyesha ni namna gani anavyokubali sanaa yake.

Davido amempatia zawadi ya mkufu msanii mwenzake aitwae Zlatan wenye gharama ya Sh.milioni 19.

Kutokana na tukio hilo, mitandao ya kijamii wiki nzima imekuwa ikijadili suala hilo huku wafuasi wa mwanamuziki huyo wakimpongeza kwa kitendo chake hicho.

Hata hivyo, Davido ameacha maswali yasiyokuwa na majibu kwa mashabiki huku wengine wakisema huenda Davido ana mpango wa kumsaini msanii huyo katika lebo yake.

Davido na Zlatan hapo awali walishawahi kufanya wimbo wao wa pamoja uitwao Bum Bum.





SHILOLE



SHAMSA



AUNT



WEMA

WANAPIGA PESA

## Kupitia ustaa, urembo wao

**Na Adam Fungamwango**

UMAARUFU ni kitu ambacho binadamu wengi hupenda kuwa nao. Tatizo ni kwamba hauji hivi hivi tu, lazima ifanyike kazi ua ziada na mhusika kujenga jina.

Wakati mwingine umaarufu huja tu kutokana na kipaji halisi kilichotoka kwa Mwenyezi Mungu. Hiki huwa hakifi na hakinyang'anywi na binadamu yoyote hadi pale mwenye nacho ataondoka na kipaji chake duniani.

Umaarufu pia humfanya mtu kupata urahisi wa mahitaji yake muhimu ambayo yangemgharimu pesa nyingi, muda mwingi kuyapata.

Hapo hapo, kuna mastaa hujiongeza na kutaka kujiongezea kipato nje ya kazi yake ya kipaji.

Tumeona upande wa waigizaji wa kike, wengine wao baada ya kupata ustaa, wakaamua kujiongeza na wakautumia ustaa wao kufanya kitu kingine cha kujiongezea kipato.

**WEMA SEPETU**

Ni mrembo aliyekuwa Miss Tanzania ambaye aliamua kujiingiza kwenye masuala ya uigizaji. Aliingizwa kwenye fani hii na msanii maarufu wa bongo fleva wakati huo, Steven Kanumba. Wema Sepetu mpaka sasa amecheza filamu nyingi na kuzidi kujiongezea umaarufu.

Kwa sasa anautumia umaarufu wake kujiingizia kipato kwa kazi zake mbalimbali nje ya bongo fleva na kuna wakati aliunda kampuni yake ya uigizaji.

**SHILOLE**

Huyu ni mrembo mwenye vipaji vingi. Ni mwigizaji na akapata umaarufu kwa kazi yake hiyo. Lakini baadaye akageukia kwenye muziki wa kizazi kipya. Huko nako akafanya vizuri kiasi chake.

Shilole baada ya kupata umaarufu akajiongeza. Kwa sasa amefungua mgahawa na umekuwa maarufu tu kutokana na kumilikiwa na mtu maarufu.

**JENIFER KYAKA ODAMA**

Ni mwigizaji mrembo kwenye uwezo wa hali ya juu, si tu kuigiza, lakini hata kupambana kimaisha.

Baada ya kufanya kazi kubwa ya kutumikia filamu za kukodishwa na kulipwa ambazo kwa kiasi kikubwa ndizo zilizompatia umaarufu kwa sasa ameunda kampuni yake ambayo imekuwa ikitengeneza filamu mbalimbali.

Odama ambaye kwa sasa ndiye bosi anayechukua wasanii na kuwalipa kama alivyokuwa anafanya yeye zamani, lakini pia yeye na kampuni yake wamekuwa wakiibua vipaji vipya kwa vijana wapya.

**SHAMSA FORD**

Mwanadada mrembo na mwigizaji ambaye alitamba mno kwenye tasnia ya bongo movie.

Ni mmoja wa waigizaji ambao wameutumia umaarufu wao vizuri kwani amefungua duka kubwa la nguo ambalo amekuwa akilisimamia nje ya kazi yake ya uigizaji.

**AUNT EZEKIEL**

Ni mwigizaji mrembo, mtoto wa mchezaji wa zamani wa Simba na timu ya taifa miaka ya '80, Taifa Stars, Ezekiel Grayson 'Jujuman'. Huyu pia ni kama Wema Sepetu, alianzia kushindana kwenye urembo, lakini hakubahatika kushinda kama mwenzake. Akaamua kujiingiza kwenye uigizaji kabla ya kuwa staa kama baba yake. Kwa kuutumia ustaa wake vizuri na kujiongeza, kwa sasa ni mfanyabiashara mkubwa tu jijini Dar es Salaam.

# Vijimambo

PICHA ILIYOPITA



1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.**

PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0785652621**



# Battery For Love Fukara aliyegeuka lulu

**Na Adam Fungamwango**

TANGU enzi na enzi, fukara hathaminiki. Watu wanashindwa kujifunza kumthamini mtu ambaye hana kitu. Hawatambui kuwa umasikini si kilema ambacho mtu anakuwa nacho milele. Umasikini ni kitu ambacho huenda kisikae kwa mtu huyo milele. Ndiyo maana masikini anaweza siku moja akawa tajiri na tajiri akafilisika na kuwa masikini.

Mtunzi wa filamu ya 'Battery For Love' anajaribu kulianika hili na kuiasa jamii kuondokana na tabia ya kuwadharau na kuwanyanyapaa watu wasio na uwezo. Wasanii walicheza picha hili ni Hemed Suleiman, Mazee Magari, Patcho Mwamba na wengine wengi.

Inaanza kwa kumuonyesha kijana Alex anaishi kwa kuuza chips. Anampata msichana mrembo aitwaye Jackline anayetoka kwenye familia ya kitajiri.

Mapenzi yao yanakuwa motomoto kiasi cha kuamua kutambulishana kwa wazazi. Wakati huo huo kuna kijana mtanashati Hemed anaanza kumrubuni msichana Jackie. Pamoja na utanashati wake, lakini pia ana wadhifa kazini, hivyo inakuwa rahisi tu kumrubuni msichana huyo.

Ghafla Jackie anaanza kubadilika. Anaanza kumchukia Alex na kumnyanyapaa kwa sababu ya ufukara wake. Anapokwenda kumuulizia kwao anajibiwa na kifedhuli na mama Jackie, tofauti na zamani ilivyokuwa.

Siku moja anaitwa kwenye kikao nyumbani kwa kina Jackie. Chochote kizuri alichofikiria hakikuwa hivyo. Anachokipata huko ni kutolewa maneno ya kejeli, kudhalilishwa, huku Mzee Magari ambaye ni baba mzazi wa Jackie akimwambia binti yake kuwa, mtu msomi kama yeye hawezi kuolewa na kijana masikini na asiye na elimu kama Alex.

Hatimaye Alex ambaye alikwenda na rafiki yake alifukuzwa kama mbwa ukweli. Hii ilimuumiza Alex kiasi cha kulazwa hospitalini.

Siku isiyo na jina anakutana na rafiki ya marehemu baba yake, Patcho Mwamba. Patcho anamshangaa kijana kuwa katika hali ile wakati anafahamu kuwa baba yake alikuwa tajiri.

Alex anamwambia Patcho kuwa baba yake alipofariki ndugu aliuza mali zote na kumdhulumu.

Kwa huruma, Patcho ambaye alikuwa hana siku nyingi akitokea Marekani, anamchukua na kumpeleka nyumbani kwake.

Wale ambao walidhani mwanzo kuwa Alex si msomi walikosea. Baba yake kabla hajafa alimsomesha haswa akahitimu, ila ile hali mbaya alikuwa nayo kutokana na kuathirika kisaikolojia kwa kudhulumiwa haki yake.

Anachofanya Patcho anampa Ukurugenzi kwenye kampuni yake. Binti ya Patcho naye anaonekana kumpenda Alex. Baba yake hana kipingamizi, hivyo Alex na binti ya Patcho wanakuwa wapenzi.

Upande mwingine, Hemed anafukuzwa kazi kutokana na ulevi. Anaamua kwenda kutafuta kazi kwingine. Anakwenda kwenye kampuni anayoiongoza Alex ambaye sasa amebadilika.

Ana madaraka na mke mrembo pia. Hemed anaambiwa ili apate kazi anatakiwa kwenda kesho yake na mdhamini. Anaamua kwenda na mkewe. Alex anatoka nje kutazama mfanyakazi wake na mdhamini. Anakutaka na mpenzi wake wa zamani Jackie. Ndipo Alex anapogundua kuwa Hemed ndiye aliyeleta matatizo yote yale. Pamoja na aibu aliyopata Jackie na Hamed, Alex anawaambia wasiondoke. Anamwambia Hemed kuwa kazi amepata, yeye hana kinyongo na yaliyopita yamepita.



KALITIKISA

# Zari awaka kisa manukato

AMA kweli umaarufu huleta heshima! Ndivyo Staa na mrembo Afrika Mashariki, Zarina Hassan maarufu kama The Boss Lady wiki hii alipojenga heshima baada ya kulitetemesha shirika la ndege la Kenya na likatikisika.

Zari ambaye amejipatia umaarufu zaidi baada ya kuzaa na mwanamuziki Diamond Platnumz na kuzaa naye watoto wawili, alibwatukia shirika hilo akilalamika kuibiwa vitu vyake ndani ya ndege yao.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Zari alitoa taarifa za kupotea kwa vitu vyake vilivyokuwa vikisafirishwa na ndege ya Kenya Airways.

Alilalamika kwamba anaamini vitu vyake hivyo viliibiwa ndani ya ndege hiyo, hivyo amekuwa hana furaha kutokana na tukio hilo.

Alilalamika vitu vyake vya thamani ikiwamo manukato na nguo alizotumiwa na marafiki zake kutokea Dubai zimeyeyukia ndani ya ndege hiyo na haijulikani nani amechukua.

Baada ya kutoa tangazo hilo, wafuasi wake waliwasha moto mtandaoni na kusababisha shirika hilo limjibu Zari kupitia mtandao na kumtaka ajitokeze ili uchunguzi ufanyike mara moja.

'Kwako zari, tunatamani kwa wateja wetu wote kuwa na safari nzuri, tumekutafuta ili kuweza kupata maelezo yako ambayo yataweza kutusaidia kuratibu pamoja na uongozi vitu ambavyo vimetokea katika viwanja vyetu (JHB, JKIA, EBB) ili kuweza kujua kilichotokea, tunasubiria jibu lako' ailiandika Kenya Airways.

Ombi la shirika hilo lilipokelewa vizuri na Zari na aliwashukuru kwa hatua hiyo.

'Asante sana' Zari aliandika kwa ufupi.

Pamoja na shirika hilo kujitokeza haraka na kuhitaji ushirikiano kutoka kwa mrembo huyo, mashabiki wake bado wanaendelea kutoa povu kwa kulitupia lawama ya uzembe.



# Beyonce awaumiza watu kwa urembo

MWANAMUZIKI maarufu wa Marekani, Beyonce, ametajwa kuwa mwanamke anayeshika nafasi ya pili kwa urembo duniani.

Katika tafiti zilizofanywa na Golden Ratio Of Beauty, mwanamitindo Bella Hadid, ndiye anashikilia nafasi ya kwanza.

Katika tafiti hiyo walizingatia zaidi uzuri wa umbo, midomo ya kuvutia, pua, shingo na mikatiko ya viungo.



## Funke kukanyaga Ikulu ya Nigeria

MWIGIZAJI nyota wa Nollywood, Funke Adesiyan ameteuliwa kuwa msaidizi wa mke wa Rais wa Nigeria, Aisha Buhari, katika upande wa misaada ya kijamii.

Funke atawajibika kumsaidia mke wa kiongozi huyo katika kuangalia misaada yote inayotolewa inayolenga watu maskini na wasiojiweza.

Staa huyo ameungana na watu wengine wanne waliotangazwa Oktoba 16, mwaka huu na majina yao kupitishwa na Rais Buhari.

## Regina mumeo atakuponza

REGINA Daniel na mumewe hatimaye wamezungumzia kwa mara ya kwanza maisha ya ndoa yao.

Hivi karibuni mwanablog, Daddy Freeze, aliwakuta wanandoa hao Dubai na hapo mwigizaji huyo wa Nollywood (59) aliweka wazi kwamba mume wake huwa hataki kuona anaingia jikoni kupika chakula.

Kulingana na msanii huyo amejaribu kupika peke yake lakini anashindwa kutokana na mume wake huyo ambaye ni bilionea kumwambia aache na badala yake anaingia mwenyewe.





## Simi kweli wewe mjamzito?

MWANAMUZIKI Simi ameibua mjadala mkali kwa mashabiki wake ambao wanajiuliza kama msanii huyo mjamzito au la, kutokana na picha aliyoiposti kupitia ukurasa wake wa Instagram kuwa yenye utata.

Swali kama Simi amepata ujauzito bado gumu kupata jibu licha ya msanii huyo kutimiza miezi tisa tangu afunge ndoa na Adekunle Gold.

Katika ukurasa wake wa Octoba 14, Simi aliweka picha ambayo ilimuonesha tumbo lake limekua kiasi na kusababisha gauni alilovaa kumbana.

## Helen pole yako mama

STAA wa filamu kutoka Marekani, Helen Hunt, amenusurika kifo baada ya gari lake aina ya SUV kupata ajali katika jiji la Los Angeles.

Ajali hiyo iliyotokea Oktoba 15 mwaka huu imemuacha msanii huyo na majeraha ambayo yalimfanya kukimbizwa hospitalini kupata tiba.

Kulingana na mtandao wa TMZ, Hunt alikuwa peke yake ndani ya gari wakati ajali hiyo inatokea.



SAFU



Na John Juma
0716217615

MIONZI YA SHERIA

# Inakuwaje wazee kuhoji mahakamani?

KWA wanaokuwa mahamakani iwe kwenye kesi zao, za jamaa zao au nyingine, wakati mwingine wanaweza kujiuliza hivi kuna uhalali wazee wa baraza wanaosikiliza kesi kumhoji shahidi maswali mahakamani?

Kwa mujibu wa kifungu cha 265 cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai, kinaelekeza kuwa kesi zote za jinai mahakama kuu ziendeshwe kukiwa na usaidizi wa wazee wa baraza, kadhalika kifungu cha 7 cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu kinataka vivyo hivyo kwa upande wa mahakama za mwanzo.

Kifungu cha 177cha Sheria ya Ushahidi kinaruhusu wazee wa baraza kuuliza maswali mashahidi wakati wa kesi. Huku kifungu cha 290 cha Sheria ya Ushahidi kikiruhusu hayo kufanyika, aidha wakili na wahusika katika kesi kwa maana ya mshitaki na mshitakiwa kuhojiana maswali pia ni jambo linaloruhusiwa.

Kifungu cha 177 kinawaruhusu wazee wa baraza kuuliza maswali wakati tukiona hiki cha 290 kikiruhusu wakili pamoja na mshitaki na mshitakiwa kuhojiana maswali. Kisheria kuna tofauti ya kuhoji maswali(cross examine) na kuuliza maswali au kwa lugha inayotumika mahakamani 'ask or put questions.

Na tofauti ni hiyo kuwa katika vifungu hivi wazee wa baraza wameruhusiwa kuuliza, wakati mawakili na wahusika wa kesi wakiruhusiwa kuhoji.

Katika mahakama kuhoji ni kuuliza maswali ya kumchanganya shahidi, maswali ya mitego, maswali yaliyo nje na muktadha wa kesi ili kumvuta shahidi na maswali mengine ambayo hayajanyooka. Hata maswali yaliyonyooka yanaruhusiwa pia katika kuhoji. Anayehoji au kwa lugha ya kortini cross examine, ana uwanja mpana wa kuhoji chochote. Kwake mbingu ndio mpaka wa kuhoji na anaamini kuwa huku ndiko kuhoji.

Vilevile, kuuliza maswali kwa mujibu wa tafsiri ya kifungu cha 177 Sheria ya Ushahidi ni kuuliza maswali yaliyonyooka tu na kuepuka swali lolote lenye lengo la kumchanganya shahidi. Ni maswali yanayolenga kupata ufafanuzi tu katika kile alichosema shahidi huyo.

Hii ndiyo tafsiri iliyotolewa na majaji watatu wa mahakama ya Rufani Jaji January Msoffe,Rutakangwa na Jaji Bwana katika Rufaa namba 147/2008 kati ya Mathayo Mwalimu na Masai Rengwa dhidi ya Jamhuri.

Ni makosa wazee wa baraza kuvaa joho la uwakili au joho la mshitaki na mshitakiwa na hivyo kuanza kuhoji maswali. Hii imekua kawaida sana hasa mahakama za mwanzo ambapo wazee wa baraza wamekuwa wakihoji kufikia hatua ya kupandisha jazba kana kwamba naye ni mhusika katika kesi.

Lakini pia wamekuwa wakihoji watuhumiwa katika staili ya uwakili. Yote haya ni makosa.

Iwapo jambo kama hili limekuta basi hii inaweza kuwa sababu ya rufani kwa kuwa unahisi hukutendewa haki kwa kuhojiwa na wazee wa baraza.

Wazee wa baraza wanatakiwa kubaki na kazi yao ambayo ni kuuliza, kushauri huku kazi ya uwakili ya kuhoji na ile ya kuamua ya uhakimu au ujaji kuwaachia wenyewe. Wakati mwingine watuhumiwa hufokewa na wazee wa baraza. Hii si sawa na yafaa ifahamike hivi ilivyoelezwa kuwa si jukumu lao kufoka.

Kitu ambacho unaweza kufanya kama wewe ni mtuhumiwa na mzee wa baraza akakuhoji, au kupaza sauti kwa ukali yafaa umueleze kuhusu wajibu wake na uombe mahakama iyaandike na kuyaingiza kwenye kumbukumbu hayo uliyomueleza.

Na usisitize yaandikwe kweli kwakuwa iwapo utapatikana na hatia hayo yanaweza kuwa sababu yako ya rufaa.

Ni vyema pia kufahamu kuwa mahakama ya rufani katika kesi iliyotaja hapo juu imeshauri muda wa wazee wa baraza kuuliza maswali. Sio wakati wote watauliza maswali bali katika muda maalum. Mahakama ya Rufani imependekeza wazee kuuliza maswali mwishoni kabisa baada mawakili kufunga kumhoji shahidi(re-examination) au kama hakuna mawakili baada ya mshitaki na mshitakiwa kumaliza kuulizana maswali.

Wasiulize muda wowote au kumuingilia na kumkatiza shahidi wakati akieleza au akijibu swali. Wasubiri wanaohojiana wamalize ndipo waje kuuliza. Majaji hawa wabobezi wanashauri wazee kuyazingatia haya.



Na Reubeni Lumbagala

KALAMU YA MWALIMU

# Mmomonyoko wa maadili ulivyochoma shule

HIVI karibuni, wanafunzi wa kidato cha tano na sita wa Sekondari ya Kiwanja wilayani Chunya mkoani Mbeya, walichapwa viboko na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila akiwaadhibu kwa kuchoma mabweni mawili.

Tukio hilo linatokana na wanafunzi hao kuchukuliwa simu zao na uongozi wa shule wakionywa kuvunja sheria na kanuni za shule zinazowakataza kumiliki simu wakiwa shuleni.

Wanafunzi hasa wanaosoma shule za bweni, wamewekewa utaratibu mzuri wa kuwasiliana na wazazi, walezi na ndugu zao kupitia namba za simu za walimu walezi wa kiume na wa kike. Uwepo wa utaratibu huu unatumika badala ya wanafunzi kumiliki simu wakiwa shuleni. Taratibu hizo zimewekwa kwa kutambua kuwa upo uhitaji wa wanafunzi hao kuwasiliana na ndugu lakini sharti mawasiliano hayo yafanyike kupitia simu za walimu wao.

Kwa mantiki hii, mwanafunzi kumiliki simu wakati sheria na kanuni za shule zimekemea jambo hilo ni utovu wa nidhamu na kukiuka sheria na taratibu za shule ambazo adhabu yake ni pamoja na kufukuzwa shule pale itakaposhauriwa.

Walimu wa Sekondari ya Kiwanja walisimamia sheria na kanuni za shule kwa kuwapokonya wanafunzi hao simu ambao nao walipaswa kuwa wapole na kukubali kuwa wamefanya makosa ili waepukane na adhabu ya kufukuzwa shule kufuatia kosa lao la kumiliki simu shuleni.

Kinyume chake, wanafunzi hao waliishia kuchoma moto mabweni mawili wa shule ya na kuteketeza kila kitu.

Ni jambo la kusikitisha kuona wanafunzi wa kidato cha tano na sita wenye uelewa mkubwa wa mambo kufanya majanga kama hayo ya kuharibu miundombinu ambayo ni mali ya umma kwa makusudi.

Hakuna jambo lolote ambalo linaweza kuhalalisha kuharibu mali ya umma kama walivyofanya wanafunzi hawa kuchoma moto mabweni.

Sasa, ukipima kosa la uchomaji wa mabweni na sababu ya wanafunzi kuchoma moto hayana uhusiano hata kidogo. Yaani wanafunzi wafanye kosa la kumiliki simu, hatua dhidi yake ichukuliwe kwa kuwanyang'anya , halafu wanafunzi waamue kuchoma mabweni moto, haiingii akilini hata siku moja.

Kama nilivyotangulia kusema kuwa hakuna sababu yeyote inayoweza kuhalalisha wanafunzi au yeyote yule kuchoma shule. Gharama kubwa zinatumika katika ujenzi wa shule na miundombinu yake yote kama mabweni, ofisi, mabwalo na vyoo.

Gharama hizi zinatokana na kodi zinazolipwa na wananchi pamoja na misaada ya wadau na wahisani wengine wa sekta ya elimu. Hivyo basi, suala la kutunza miundombinu na mali mbalimbali za serikali na za sekta binafsi ni jambo la lazima kisheria na si hisani.

Laiti wanafunzi hao wangekuwa na maadili na nidhamu wasingefikia uamuzi ya kuchoma shule moto. Watoto hawa wametoka ndani ya familia ambazo ndizo taasisi ya kwanza ya malezi ya watoto.

Katika ngazi ya familia, malezi na maadili bora ni lazima yaimarishwe badala ya kuwaachia walimu peke yao ambao wanawapokea watoto kutoka katika familia.

Serikali inatumia fedha nyingi katika uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya shule. Jambo ambalo wanafunzi hao wanapaswa kulithamini kwani hata wao wenyewe wasingepata nafasi ya kusoma katika shule hiyo kama kusingekuwa na miundombinu ya elimu.

Hivyo basi, kuharibu mali za shule kwa kuchoma mabweni moto ni kurudisha nyuma jitihada za serikali katika kuboresha elimu.

Kama taifa, tunapaswa kujiuliza tumekosea wapi katika malezi ya watoto wetu. Ni kutokana na ukweli kuwa, baadhi ya watoto wa sasa wamekosa maadili na nidhamu na hivyo kuwa katika hatari ya kujenga taifa la watu wasio na nidhamu.

Jamii isiyo na heshima, nidhamu na maadili haiwezi kusonga mbele kimaendeleo.

Wanafunzi wengine wanapaswa kujiepusha na makosa yaliyofanywa na wenzao wa Sekondari ya Kiwanja kwa kuhakikisha kuwa wanatii sheria, kanuni na miongozo ya shule ili kujiepusha na adhabu ambazo zinakwepeka. Wazingatie yale wanayoelekezwa na walimu kwani walimu wapo kwa ajili ya kuwahudumia, kuwalea na kuwafundisha tabia njema kwa mustakabali mwema wa maisha yao ya sasa na ya baadaye.

Aidha, wazazi na walezi tuhakikishe kuwa tunawalea watoto wetu katika misingi ya kuwa na tabia njema ili kusaidia kujenga taifa la watu wenye kuheshimu sheria za nchi kama ilivyo wajibu wa kila raia mwema wa nchi.

Wanafunzi wa Sekondari ya Kiwanja, warejeapo shuleni, wafungue ukurasa mpya wa mahusiano mazuri pamoja na walimu wao, wazidishe juhudi katika kujisomea ili waweze kufanya vizuri katika masomo yao na hatimaye kupata nafasi ya kuendelea na elimu ya juu. Tafakari.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

**Kwa maoni na ushauri: (+255) 764 66349.**

# Ndivyo Mwalimu huyu anavyomuenzi Nyerere

**Na Sabato Kasika**

OKTOBA 14 mwaka huu, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, ametimiza miaka 20 tangu alipofariki dunia huko London, Uingereza.

Licha ya kukumbuka siku alipovuta pumzi yake ya mwisho, Watanzania wana mengi ya kujifunza, kutokana na vitu vingi ambavyo shujaa huyu amevifanya enzi ya uhai wake, tangu alipoanza harakati za kutafuta uhuru wa nchi hii mwaka 1961.

Mmoja wa watu hao ni mwalimu na Meneja wa Shule ya Sekondari Efforts iliopo Bagamoyo mkoani Pwani, Othiniel Mnkande, ambaye anazungumzia uamuzi wa Baba wa Taifa kuacha kazi ya ualimu na kujiingiza katika siasa.

“Kiumri mimi bado ni kijana na lakini nimejua habari za Baba wa Taifa , ukweli ni kwamba nilipenda sana kufuatilia na kujua historia yake na jinsi alivyojishughulisha kwa ajili ya taifa hili,” anasema Mnkande.

Vile vile, anasema tangu anaanza elimu ya msingi alikuwa anafuatilia habari zake na alivutiwa na uzalendo aliokuwa nao kwa taifa na Watanzania kwa ujumla. Tena yeye ni miongoni mwa wafuasi wakereketwa wa Nyerere.

“Mwaka 2000 nikiwa kidato cha sita nilifanya mradi wangu kuhusu mambo ya ujamaa na kulazimika kutembelea nyumbani kwa Mwalimu Nyerere kijijini Butiama na kuelezwa jinsi alivyokuwa akiishi bila kujivuna,” anasema Mnkande.

Mwalimu huyo anasema ingawa alikuwa hapendi ualimu, alijifariji kupitia kwa Nyerere, kwa vile alikuwa mwalimu na hatimaye Rais wa kwanza wa Tanzania na kwamba unaweza kuwa yoyote kupitia taaluma ya ualimu.

Mwalimu huyo anasema, mbali na mengi, ambayo Baba wa taifa alifanya, anafarijika kwa jinsi alivyofanya maamuzi magumu ya kuacha ualimu na kuingia katika siasa ili kupigania uhuru wa Tanzania.

“Hebu wewe fikiria kwamba TANU haina mshahara, lakini Mwalimu Nyerere anaamua kuacha kazi ya mshahara na kukubali kuingia kwenye siasa...huu mimi ninauona ulikuwa ni uamuzi mgumu mno,” anasema.

Aidha, uamuzi huo ndiyo ulioleta uhuru wa Tanzania na inawezekana bila kufanya maamuzi magumu huenda wakoloni wasingeachia madaraka mapema.




Mwalimu Nyerere akibebwa na wananchi, kufurahia ukombozi wa Tanzania mwaka 1961.**PICHA: MTANDAO.**

**HALI ILIVYOKUWA**

Anasema, alifuatilia historia ya Baba wa Taifa jinsi alivyopewa kazi ya kufundisha katika Sekondari Pugu Oktoba 9, 1952 baada ya kumaliza masomo yake katika Chuo Kikuu cha Edinburgh,Uingereza.

“Februari mwaka 1955, Mwalimu Nyerere akiwa kiongozi wa TANU, alikwenda New York, Marekani katika Umoja wa Mataifa kuhutubia Baraza la Wadhamini la Umoja wa Mataifa, kwa nauli ya Sh. 12,000, zikiwa ni fedha zilizochangwa na wanachama kwa muda mfupi,” anasema.

“Wakati huo Tanganyika ilikuwa chini ya Udhamini wa Umoja wa Mataifa na Uingereza ilikuwa inatutawala kwa niaba ya umoja huo. Agosti 1954 ulikuja ujumbe kutoka Umoja wa Mataifa, kukagua utawala wake unavyoendeshwa na kutoa taarifa kamili kwenye baraza lake la wadhamini ikiwa ni moja ya desturi za kila baada ya miaka miwili ujumbe kuja.” Anakumbusha.

Anaeleza kuwa, TANU ilifurahishwa na taarifa hiyo ikaamua kupeleka ujumbe wake huko kwenye Wadhamini wa Umoja wa Mataifa wakati taarifa hiyo ingejadiliwa, na kwamba Mwalimu Nyerere akachaguliwa kwenda kufanya kazi hiyo.

“Gavana aliposikia habari hizo akashtuka sana.Yeye na serikali ya Uingereza kwanza hawakuipenda taarifa ya Ujumbe wa Umoja wa Mataifa. Pia kusikia TANU inapeleka mjumbe New York, na mjumbe mwenyewe ni Julius Nyerere,” anasema,

Mwalimu Mnkande .

Anakumbusha kuwa Gavana naye aliamua kupeleka ujumbe mzito wa watu watatu wa kumpinga Nyerere na kwamba jambo hilo lilipitishwa haraka katika baraza la kutunga sheria (Legco).

“Baada ya mkutano huo Legco wajumbe watatu Waafrika walipanda gari na kurudi pale walipokuwa wamefikia.Hiyo ilikuwa Februari 10, mwaka 1955,” anasema.

Mwalimu Nyerere aliporudi alikuta tayari wakoloni wameshajiandaa kumtoa katika uongozi wa TANU kwa njia ya hila, ambazo hata hivyo alizing’amua na kuchukua maamuzi magumu.

**ALICHOAMUA**

Anasema Mwalimu Nyerere akiwa kiongozi wa TANU, wakoloni walipanga mtego wao na mkuu wa shule ya Pugu, kwamba atakaporudi kutoka New York apewe kuchagua mojawapo kati ya mawili.

“Kimsingi ni kwamba uwezo wa Nyerere uliwashtua viongozi wa kikoloni hadi wakalazimika kumpa mtego huo wa kuchagua kati ya siasa na kazi ya ualimu, lakini mwisho wa siku akafanya maamuzi magumu,” anasema.

Anasema Mnkanda kuwa , uchaguzi huo aliopewa Mwalimu ulikuwa ni kufanya kazi ya ualimu na kuacha kujihusisha na siasa au afanye siasa tu aache kabisa ualimu kazi ambayo ilikuwa ni ajira yake.

“Walifanya hivyo kwasababu walijua wazi kuwa TANU haikuwa na fedha ya kumlipa mshahara. Mwalimu Nyerere alirejea kutoka New York Jumamosi Machi 21 mwaka 1955 jioni,” anasema.

Anafafanua kuwa kesho yake mkuu wa sekondari alimwita Nyerere ofisini na kumwambia, jinsi alivyokuwa akijishughulisha sana na siasa, isingewezekana kumruhusu aendelee na kazi ya ualimu, hivyo alimwita achague moja kati ya mambo hayo mawili.

“Mwanangu Julius, ualimu na siasa havipatani hata kidogo, fuata oni langu, uache kabisa mambo ya siasa na uzingatie kazi yako ya ualimu”.

Mwalimu Nyerere alitoka nje, fikra zimemjaa kichwani, akaenda nyumbani akayafikiri maneno hayo na akajiuliza afanye nini sasa. Lakini haikuchukua muda mrefu akapiga moyo konde akamwendea mkuu wa shule.”

Anasema, pamoja na vitisho hivyo, Mwalimu Nyerere alifanya kitendo cha ushujaa na busara kwa kumpa mkuu wa shule barua ya kujiuzulu kazi ya ualimu na kuingia rasmi kwenye siasa.

Uamuzi wa Mwalimu Nyerere ndiyo ambao ulisababisha kushika nafasi mbalimbali za uongozi hadi kufikia kiongozi mkuu wa nchi hadi alipong’atuka rasmi mwanzoni mwa miaka ya 80.

**KUNG’ATUKA**

Anasema Mwalimu Nyerere ni kati ya viongozi wachache wa Afrika ambao wameacha madaraka kwa hiari baada ya kutawala kwa muda mrefu, akiwa bado anapendwa na wananchi walio wengi katika nchi.

“Alipostaafu urais mwaka 1985 alirudi kijijini kwake Butiama, ambako aliendesha shughuli za kilimo lakini aliendelea kuwa na umuhimu katika siasa za Tanzania hadi kifo chake,” anasema.

Mwalimu Mnkande anasema, Nyerere ni mwasisi wa itikadi ya ujamaa na kujitegemea iliyotangazwa hasa katika Azimio la Arusha, ambayo Mnkande, anaamini kuwa hata sasa bado ina umuhimu mkubwa kuleta maendeleo.

# Vijiwe vya ubaya wa wagombea vya nini?

Na Gaudensia Mngumi

MARA nyingi wakati wa uchaguzi uwe wa serikali za mitaa au mkuu wengi wanaanzisha kampeni vijiweni za kushiriki kwenye kuwabomoa badala ya kuwajenga walioonyesha nia.

Kuanzia sasa hadi Novemba 24, uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji ndiyo habari ya mjini. Uchaguzi umewadia na sasa hilo ndilo linakuwa gumzo muhimu kwenye vijiwe vingi sehemu za mijini.

Habari za uchaguzi zinavuma na majina ya wagombea au walioonyesha nia yanachambuliwa. Kila kiongozi anayetaka kugombea watu wanamsaka ili kuibua kila baya alilofanya au analolifanya sasa.

Wapinzani wake wanaangalia na kusikiliza alilosema na analolizungumza leo.

Cha kushangaza ni kwamba mabingwa hawa wa masuala ya siasa na ya mahusiano ya kimataifa ambao ni wanasiasa ndani ya upinzani na hata ndani ya CCM wamejikita mno kujadili udhaifu wa kiongozi mpya ambaye pengine ameonyesha nia ya kutaka kugombea uongozi kwenye uchaguzi huu wa serikali za mitaa.

Inavyoonekana kuna wengi wenye nia ya kuwaharibia wenzao wakidai kuwa hawafai kubeba jukumu hilo kwa kila nyanja na kuwashawishi wapiga kura kwamba hawafai kukiongoza kijiji, mtaa au kitongoji.

Watu wanajadili zaidi kuhusu ubovu na udhaifu wake, wanamkosoa muhusika mmoja mmoja na mipango yake anayotarajia kuizungumzia kwenye kampeni za uchaguzi huo.

Kama alikuwa kiongozi kwa miaka mitano iliyopita wanazitafuta na kuibua kashfa zake.

Pengine wanasababu . Lakini kwa ujumla si wakati wa kuchafuana.

Huenda kila mmoja anataka asikie habari njema kuwa mgombea ataondoa wizi, vibaka na kufanya operesheni za kutokomeza umaskini kwa kuanzisha vikundi na miradi ya wajasiriamali.

Ni jambo jema lakini ni aibu kuwa kwenye vijiwe vingi zama hizi za kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa ndiko kuna mabingwa wa kumsema mgombea flani.

Pamoja na 'kumnanga' mgombea wanakijiwe wanasahau kuwa kuna mambo yanawahusu ambayo walitakiwa kuyasema na kumshauri mgombea ili ayazungumze na kuyafanyia kazi.

Ukifika kijiweni hayo mara nyingi hawayasemi wala hawamshauri mgombea afanye nini kuondoa kero hizo.

Kwa mfano, watu wanaweza kumfuata na kumweleza kiongozi wao mtarajiwa ama aliyeko madarakani, jinsi ambavyo wanakerwa na uzembe kwenye maeneo ya kiutendaji na kwa ujumla ubovu wa viongozi au kiongozi huyo.

Ndivyo wananchi wanavyotakiwa kusimama na kueleza uzembe au ubaya wa watu wanaowaona wanagombea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Kazi ya kuwakosoa wanaogombea ni jambo jema lakini si kuchafuana mitaani au kwenye vijiwe. Ni vyema kuchukua hatua wenyewe ya kuwarekebisha wanaokosea kwenye mikutano pengine ya vyama au hata ya kijiweni badala ya kuanza kusemana ovyo mitaani. Vilevile badala ya kuwasema wagombea wa serikali za mitaa ni wakati wa kumshauri jinsi kiongozi anayetaka kugombea uongozi atakavyokosoa na kuchukua hatua dhidi ya mtu aliyepora wenzake ardhi na kusababisha migogoro ya wakulima na wafugaji kwenye vijiji vyetu.

Ni vyema pia kumhoji na hata kumshauri jinsia ambavyo atakabiliana na rushwa kwenye masuala mengi yanayohitaji saini za viongozi wa serikali wa mitaa hasa kwenye masuala ya kuuza ardhi, nyumba na mali nyingine ambazo viongozi hao wanahusika.

Tunataka kuona wachambuzi wa masuala ya kisiasa na ya kiongozi wakiwahoji viongozi wa serikali za mitaa watafanya nini kuzuia mabinti wasipate mimba na kuwasaidia wasome na kumaliza shule za msingi hadi kidato cha sita.

Aidha, tunataka kuona watu wakimbana kiongozi anayegombea ili aeleze jinsi atakavyosaidia kutumia rasilimali zinazopatikanaji kijijini kuongeza pato la wananchi na kuwawezesha kuondoka kwenye umaskini na kukosa tumaini.

Aidha, ingependeza kama watamshauri na cha kufanya pia.

Ingependeza kwenye mikutano ya vijiweni au hadhara au ya marafiki wa mgombea, watu wakihoji na kupata majibu ni kwa namna gani kutakuwa na masoko na biashara ya faida kwa wakulima vijijini?

Ni lina wananchi wanaokaa kandokando ya barabara watakuwa na vitega uchumi na kuwa na maisha bora kutokana na ukweli kuwa barabara nyingi zinapita vijijini lakini hakuna uwekezaji wenye tija?

Ni wazi kuwa viongozi wa vijiji mitaa na vitongoji hawajaweza kutumia barabara kiujasiriamali ili kuleta maendeleo kwa wananchi wao.

Ifike wakati watu wabadilike wengi wamekalia kukosoa ya Simba na Yanga. Waamke watafute mchambuzi makini mmoja wa masuala yanayohusu hasa siasa zetu na asaidie masuala nyeti ya kuwahoji wagombea ambao wanataka ofisi za kuwatumikia wananchi.

Ingependeza mtaalamu akasaidiana nao kuhoji wagombea inakuwaje wakulima wanaumizwa na wafanyabiashara wageni kutoka nchi jirani wanaokuja kununua mazao yao tena vijijini kwenye shamba yao?

Inashindikanaje kuwazuia wafanyabiashara hao kutoka nchi jirani kuingia kwenye mashamba ya wanavijiji kununua maparachichi, machungwa, maembe na matikiti wakati viongozi wa mitaa na vijiji wapo? Kama vile viongozi wa vijiji hatuoni watu wanavyopambana kukwepa kodi kisheria na kuwaibia wananchi wetu vijijini tena nyumbani kwao?

Kwa nini wachambuzi wetu wa kukatisha tamaa msitunze nguvu ya kukosoa na kutukana wagombea wanaojitokeza badala yake muitumie nguvu hiyo kushauri masuala muhimu ya kiujasiriamali ili kuboresha maisha ya wananchi wetu vijijini?

Ni wakati wa kujenga nchi si muda wa kuona kuwa eti mgombea wa Chadema au wa CCM, ACT Wazalendo au CUF ana kasoro zipi na kuanza kuziibua.

Kinachotakiwa ni kujua kuwa kuna wakati wa kuanika nyavu na kushusha nyavu majini. Sasa tunafanya kipi kutosa nyavu au kuzikausha?

Kwa serikali za mitaa huu ndiyo muda wa kutosa nyavu kuvua samaki wengi na wanaopasua majarife.




Vijana wakiwa kijiweni au maskani ni vyema wajadiliane masuala chanya kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa badala ya kulaumu na kukosa pamoja na kukatisha tamaa wagombea. **PICHA: MTANDAO.**

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 16 00)



**Dondoo: Chini**

1. Mnyama mjanja
2. Kikundi cha dini fuani
3. Isiyokuwa nzito
4. Huchomwa na kufukizwa
5. Bunge la Urusi
6. Mtaa Dar 7. Tabawali
11. Badilisha kitu kwa fedha
13. Ukosekanaji wa hiari
14. Bomba la kuzuia maji yasienee 15. Desturi
17. Dola 20. Sehemu iliyoinuka
21. Kinyume cha tamu
22. Wingi wa neno tezi
25. Pombe

**Dondoo: Kulia**

1. Nchi iliyogawanyika Afrika
6. Dakitari
9. Baba wa Taifa 9. Pengine
10. Baini
12. Udadisi, uchunguzaji
16. Baraza la sanaa la taifa
18. Uhai
19. Soseji ya Kiyahudi
23. mdudu wa kuvulia samaki
24. Msafiri 26. Kidonda
27. Mnyama asafiriye Jangwani
28. Dhania

## Jibu Na: 15

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| G | E | N | E | V | A | | M | C | H | A | N | A |
| H | | A | | | | M | | H | | B | | N |
| A | U | S | T | R | A | L | I | A | | U | | D |
| R | | A | | I | | A | | K | A | D | H | I |
| A | M | B | I | A | | N | | A | | U | | K |
| M | | A | | L | E | G | E | Z | A | | | I |
| A | | | U | | K | O | M | A | | A | | S |
| | N | A | M | B | A | | B | | A | | | H |
| | Y | | B | | R | | E | | N | U | S | A |
| M | A | S | I | K | I | O | | K | I | M | A | |
| | N | | L | | | M | P | A | K | A | N | I |
| | D | | E | | | B | | T | A | G | A | |
| K | A | A | | M | P | I | R | A | | A | | |

SUMU KUVU

# Maofisa ugani onyesheni dawa chanzo homa ya ini, udumavu,

Na Mwandishi Wetu

SUMU kuvu (aflatoxin) ni janga la afya lililojikita kwenye vyakula vya binadamu na mifugo .

Sumukuvu ni sumu zitolewazo na aina ya ukungu kuvu (fangasi) unaoota kwenye mbegu za nafaka na jamii ya kunde, mazao ya mizizi, karanga, vyakula

na malisho ya wanyama vikiwa shambani au kwenye ghala.

Ingawa aina nyingi za kuvu zinaweza kuota na kukua katika vyakula hivi, ni wachache tu ambao hutoa kuvu aina hii ya fangasi kitaalamu hujulikana kama Aspegillus flavus na husambaza sumu kuvu ijulikanayo kama 'aflatoxins.'

Sumu hii huingia mwilini mwa binadamu au mifugo kupitia kula ya chakula kinachotokana na nafaka. Sumu kuvu haionekani kwa macho, haina harufu, ladha, wala rangi, lakini kuvu anayetoa sumu hizo anaweza kuwa na rangi ya kijani, chungwa, kijivu au njano na anaweza kutoa harufu ya kuvunda. Karibia asilimia 25 ya vyakula duniani vina maambukizi ya sumu kuvu na watu bilioni 2.5 wako katika hatari ya kudhurika.






Ndivyo yalivyo mahindi yenye kuvu, hata hivyo dawa ya aflasafe inatumiwa kutibu kuvu hao kupunguza madhara kwa binadamu. **PICHA: MTANDAO.**

### ATHARI

Kwa kuwa sumu hii huchafua mazao, inachukuliwa kama ni chanzo kikuu cha saratani ya ini hasa kwa binadamu. Sumu hii pia huharibu mfumo mzima wa kinga za mwili kwa binadamu na wanyama na hivyo kusababisha kushambuliwa kirahisi na magonjwa mbalimbali.

Watafiti wa Taasisi ya International Institute of Tropical Agriculture (IITA) huko Benin taifa lililoko Afrika ya Magharibi, wanaelezea kuwa sumu hii ni chanzo kikubwa cha kuzorota kwa ukuaji wa viumbe mbalimbali au udumavu.

Mathalani ni sababu kubwa ya kudumaa kwa watoto barani Afrika.

Baadhi ya watoto hupata sumu hii katika umri mdogo na matokeo yake kasi ya ukuaji hupungua kwa kiasi kikubwa na hali hii hudhihirika pale watoto hawa wanapoachishwa maziwa ya mama na hasa wanapokuwa kwenye hatari za maambukizi ya magonjwa mengine kama kuhara, malaria na magonjwa ya mfumo wa hewa, anabainisha Dk. Haunsa wa taasisi ya IITA.

### KWA BINADAMU:

Changamoto ya sumu kuvu ni kwamba si kwa mara zote mkulima akazitambua aina ya fangasi wanaozalisha sumu hii kwenye nafaka anazolima.

Sumu hii si rahisi kuitambua kwa macho. Lakini pia haiathiriwi na moto haiwezi kuondoka kwenye chakula hata kama kitapikwa au kuchachusa .

Hivyo upo uwezekano kwamba idadi kubwa ya watu Afrika Mashariki kuwa wameathiriwa na sumu hii sugu kama ilivyo kwa nchi za Afrika

Magharibi japokuwa takwimu kamili za ukubwa wa athari zake hazijapatikana.

Vilevile walaji wengi hawana habari kwamba wanatumia vyakula vilivyochafuliwa na sumu kuvu na hata wale ambao wananunua vyakula kwenye maduka makubwa hawakusalimika na sumu hii anasema, Dk. George Siboe.

Siboe ni mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi aliyefanya utafiti uliobaini sumukuvu kwenye bidhaa mbalimbali za unga zinazouzwa madukani.

### CHANZO CHA SUMU

Kwa kiasi kikubwa wadudu ndiyo hasa wanaochangia kusambaa kwa sumu kuvu kwenye mahindi na nafaka nyingine mashambani.

Hii inamaanisha kwamba uwepo wa idadi kubwa ya wadudu kama mende na mbungua kwenye maghala ya chakula hukaribisha uwezekano mkubwa wa tishio la janga la sumu hii.

Kwa mfano huko Afrika Magharibi imegundulika kwamba tatizo la sumu kuvu huanzia mashambani mathalani, uharibifu unaofanywa na dumuzi kwenye mazao yaliyokomaa shambani . Uharibifu huo huongeza uwezekano wa nafaka kuathiriwa na jamii ya fangasi ya ukungu na hatimaye husababisha kusambaa kwa sumu kuvu ambayo huzidi kuongezeka kadiri mashambulizi ya mdudu dumuzi yanavyoongezeka.

Hii inamaanisha kudhibiti wadudu hawa mashambani kwa kutumia njia za kibaiolojia ndiyo suluhu ya kudumu dhidi ya janga la sumu kuvu.

### UDHIBITI

Watalaamu wanashauri kulima aina za mazao zenye ukinzani dhidi ya kuvu .

Pia vuna mazao yakiwa yamekauka vizuri kama inavyoshauriwa na wataalamu na epuka kutia majeraha kwenye mazao yako

Ni vyema kuacha kuanika mazao chini kwenye udongo inashauriwa kuanika juu ya meza na utumie turubai au aina nyingine ya kifaa cha kuanikia

Aidha, wakati na baada ya kuvuna tupa mbegu au mazao yaliyooza inashauriwa pia kuhifadhi mazao mahali pakavu na pasipo na joto. Wakulima na walaji wanatakiwa kuhakikisha mazao yaliyohifadhiwa hayalowi.

Kadhalika mazao yahifadhiwe kwenye ghala linaloruhusu mzunguko wa hewa. Pia kuzuia wadudu waharibifu na kuvu kwa kunyunyiza dawa zinazoshauriwa na wataalamu.

Wanashauriwa kutumia "srerifum" hasa kwenye mahindi na maghala ya kuhifadhia nafaka.

Dawa za kibaiolojia kama vile AflaSafeTM (aina ya kuvu ambaye hukinzana na yule atoaye sumu kuvu) ni vyema kuitumia.

Inashauriwa pia kutumia dawa zinazodhibiti na kuondoa sumu kuvu wakati wa usindikaji wa vyakula vya binadamu kama vile 'mycobind' kwa upande wa wanyama.

Ikumbukwe mlaji wa bidhaa zitokanazo na mifugo na kilimo ndiye mhanga mkubwa wa madhara ya sumu kuvu.

Mlaji huyu huathirika aidha kwa kula moja kwa moja mazao kama mahindi yaliyoathirika au maziwa ya ng'ombe aliyepata sumu kuvu kupitia kulishwa malisho yaliyo na sumu hii.

Hata hivyo ni huyuhuyu mlaji ndiye anayezipa uhai sekta nzima hizi za uzalishaji kupitia mapato ya mauzo ya bidhaa hizi kwake. Hivyo kuna haja ya kumhakikishia usalama kila mlaji ili kuweza kuzinusuru sekta hizi za uzalishaji kwani kama ataangamia basi wadau wote kwenye mnyororo wa uzalishaji wataathirika pia.

### MIFUGO

Kama ilivyo kwa binadamu mifugo kama ng'ombe na kuku inapotumia vyakula vilivyoathiriwa na sumu hii kushindwa kukua vyema na hatimaye kushindwa kutoa mazao bora na kwa wingi. Vilevile upo uwezekano wa sumu hii kusambaa kwa watu kupitia kula kitoweo cha wanyama hawa.

### KULINDA WANYAMA

Tumia vichanganyio (premix) ambavyo vinasaidia kuondosha sumu hii kwenye vyakula kwa ajili ya mifugo, mojawapo wa vichanganyio hivyo ni 'mycobind na farmacid premix' ambayo huchanganywa kwenye chakula cha mifugo kabla ya kupewa mifugo. Hii inapatikana kwenye maduka ya dawa za mifugo.

### ANGALIZO

Kutokana na madhara ya afya yanayosababishwa na sumu kuvu kwa binadamu na wanyama sumu kuvu haziruhusiwi kuwepo katika mazao yaliyokusudiwa kwa matumizi ya binaadamu, mifugo, biashara na kama uwepo wake ukigundulika mazao hayo ya kilimo hayaruhusiwi kuuzwa na baadaye yatateketezwa.

Kwa kiwango kikubwa sumu kuvu huathiri biashara, faida na afya za wazalishaji na watumiaji kwa ujumla.

**Makala hii imeandikwa kutoka kwenye mtandao wa BLOG SWAHILI, KILIMO, UFUGAJI**

## HABARI KIMATAIFA

# Museveni: Bobi Wine adui wa taifa letu

**KAMPALA,** Uganda

RAIS wa Uganda Yoweri Museveni, amemtaja mkosoaji wake mwanamuziki aliyegeuka kuwa mwanasiasa Bobi Wine, kama adui wa mafanikio ya nchi hiyo.

Rais Museveni aliyasema hayo katika mahojiano na BBC.

Museveni anataka kuendelea kugombea muhula wa sita kama rais katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka 2021 baada ya kuwa rais wa nchi hiyo kwa miaka 33.

Bobi Wine, ambaye ni kiongozi wa vuguvugu la 'The People Power', anamshutumu rais huyo kwa kuongoza kwa mfumo wa ukandamizaji.

**Hatuko hapa kwa ajili ya maonyesho, hatuendi kwenye ukumbi wa michezo ya maigizo , sisi ni watu ambao tupo hapa kushughulikia masuala makubwa ya Uganda na Afrika.**

Hata hivyo, Museveni amekataa kumueleza mwandishi wa BBC , Alan Kasujja ikiwa serikali yake ni ya ukandamizaji , lakini akasema anamshughulikia Bobi Wine kama adui.

Rais huyo wa Uganda alimlaumu Wine, akisema kuwa alikwenda Marekani na kuwaambia watu wasije kuwekeza Uganda: "Unapokwenda na kuwaambia wageni kwamba hawapaswi kuja na kuwekeza katika nchi yetu, inamaanisha umeanzisha vita dhidi ya mafanikio yetu. Kwa hiyo kwa nini sasa unataka kurejea na kunufaika na mafanikio hayo?" alihoji.

Rais huyo wa Uganda alisema bado ataendelea kuwepo madarakani kwa miaka mingine zaidi kukamilisha kile ambacho yeye binafsi na wapiganaji wenzake walikipanga kukifanikisha katika nchi yao na bara la Afrika.

"Nyumba yangu inanisubiri, lakini tuna masuala kama Uganda ya kushughulikia. Ni masuala hayo ambayo yanatufanya tufanye kile tunachotaka kukifanya kisiasa pamoja na wenzetu. Kama chama tawala (NRM) kitafikiria kuwa hakihitaji mchango wa wazee basi tutaondoka madarakani kwa furaha na kufanya mambo mengine ." Museveni alimueleza mwandishi wa BBC, Allan Kasujja jijini Kampala.

"Hatuko hapa kwa ajili ya maonyesho, hatuendi kwenye ukumbi wa michezo ya maigizo , sisi ni watu ambao tupo hapa kushughulikia masuala makubwa ya Uganda na Afrika ." Alisisitiza kiongozi huyo wa Uganda.

Rais Yoweri Museveni amekuwa madarakani Uganda kwa zaidi ya miongo mitatu, amekuwa akikabiliwa na wapinzani wanaomtaka ajiuzulu na wengi wanaomtaka kufanya hivyo ni vijana na wapinzani wake .

Mpinzani wake wa muda mrefu Dk Kizza Besigye, amepitia misukosuko mingi katika harakati zake za kisiasa pamoja na mbunge Bobi Wine ambaye juhudi zake za kutumia usanii wake wa kimuziki kuhimiza ajiuzulu zimekuwa zikizimwa na maofisa wa usalama kila wakati. **BBC**

## Jeshi kudhibiti jimbo la Amhara

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

MKOA wa Amhara nchini Ethiopia unakabiliwa na hali ya sintofahamu, baada ya vifo vya watu zaidi ya 20 vilivyotokea kati ya Septemba mwishoni na mapema Oktoba mwaka huu.

Wakuu wa mkoa huo wametishia kuomba jeshi la nchi hiyo kuingilia kati ili kurejesha utulivu.

Machafuko katika eneo hilo la kaskazini mwa nchi yameendelea kutishia Amani na maendeleo kwa karibu miaka mitano.

Mamlaka ziliripoti vifo vya watu 22 tangu mwishoni mwa Septemba, kulingana na taarifa iliyotolewa na Baraza la Usalama la Mkoa wa Amhara.

Baraza hilo limezungumzia machafuko hayo kuwa ni makubwa katika ngazi ya kitaifa pamoja na vifo nyumba zilichomwa, mali ziliharibiwa na uchumi kuvurugika kwa kiasi kikubwa.

Aidha, mzozo wenye vyanzo mbalimbali, ambao unaweza kuongezeka, Baraza la Usalama la Mkoa wa Amhara, limebaini.

Baraza hilo limetangaza kuchukua hatua kadhaa, wananchi wa kawaida wamepigwa marufuku kumiliki silaha, makundi ya usalama yasiyojulikana rasmi yamepigwa marufuku na wananchi wameombwa kuwafichua wahalifu.

Vyombo vya usalama nchini Ethiopia vimewakamata watu zaidi ya 200 wakiwamo raia wa kawaida, wana usalama na wanasiasa wanaotuhumiwa kuhusika katika jaribio la mapinduzi kwenye jimbo hilo, ambako rais wa eneo hilo na mnadhimu wa jeshi waliuawa.

Mashambulizi ya mwishoni mwa juma lililopita, yalizidisha shinikizo zaidi kwa utawala wa Waziri Mkuu Abiy Ahmed ambaye ameendelea kukabiliana na changamoto za machafuko ya kikabila na mabadiliko ya uchumi wa taifa hilo.

Machafuko hayo, ambayo serikali inasema yalikuwa sehemu ya njama iliyofanywa na jenerali mmoja muasi na wanajeshi wake kuchukua udhibiti wa Amhara, yalidhihirisha namna mivutano ya kikabila inavyotishia ajenda ya mageuzi ya Waziri Mkuu Abiy Ahmed. **RADIO UFARANSA**




Waziri Mkuu wa Uingereza, Borris Johnson na Rais wa Halmashauri Kuu ya EU, Jean-Claude Juncker (kulia). **PICHA: DW**

## EU yaionya Uingereza mkataba Brexit

**BRUSSELS,** Ubelgiji

RAIS wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya (EU) Jean-Claude Juncker, ameonya juu ya kutokea hali tata zaidi iwapo wabunge wa Uingereza watashindwa kupigia kura mkataba wa Brexit uliopatikana kwa njia ngumu.

Makubaliano hayo yamepatikana baada ya takriban miaka mitatu ya kuvutana na wiki kadhaa kabla ya muda wa mwisho wa Oktoba 31 kwa Uingereza kujiondoa katika Umoja wa Ulaya.

Kazi iliyosalia sasa ni ya Bunge la Uingereza litakalo kuwa na kikao maalum leo Jumamosi kupiga kura ya iwapo liidhinishe makubaliano hayo ya Brexit au liyakatae.

Hata hivyo mpango mpya wa Waziri Mkuu Borris Johnson, unakabiliwa na upinzani katika bunge lililogawanyika huku wapinzani wake miongoni mwao kiongozi wa chama cha Leba Jeremy Corbyn, wakiukataa mkataba huo.

Aliukataa baada ya kutangazwa, na kuahidi kuwachukulia hatua wabunge wa chama hicho watakaounga mkono makubaliano hayo.

Haya yanajiri huku viongozi wa Umoja wa Ulaya wakiwa tayari kuidhinisha bajeti ya muda mrefu ya umoja huo katika siku ya pili ya mkutano wao wa kilele mjini Brussels.

Wakati hayo yakitokea kuna hali ya kutoelewana kuhusu jinsi ya kushughulikia nakisi ya ufadhili unaohusiana na suala la Brexit, na pia kuna masuala mapya yanayopaswa kupewa kipaumbele kama uhamiaji na mabadiliko ya tabianchi.

Jana , viongozi hao pia walitarajiwa kumuidhinisha rasmi aliyekuwa Mkuu wa Shirika la Fedha Duniani (IMF) Christine Lagarde, kuwa rais mpya wa Benki Kuu ya EU,

Rais mteule wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya, Ursula Von der Leyen, ambaye pia alikuwa sehemu ya makubaliano hayo ataangaziwa zaidi huku wanachama wakizungumzia masuala yanayopaswa kupewa kipaumbele katika siku zijazo na EU.

Mambo hayo yanajumuisha azma kubwa katika mabadiliko ya tabia nchi na jukumu madhubuti la kimataifa la Umoja wa Ulaya.

Von der Leyen pia anatarajiwa kuulizwa maswali kuhusu Bunge la Ulaya kuwakataa makamishna wake watatu kati ya 26. Kutokana na hali hiyo, kundi lake jipya halitaweza kuchukuwa hatamu za uongozi kuanzia Novemba 1, kama ilivyokuwa imepangwa. **DW**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# JUMBA JEKUNDU- 23

Mtunzi anapatikana (0716 350534)




Na Adam Fungamwango

NI picha ya mtu ambaye anamfahamu. Juu kulikuwa na maandishi makubwa. 'Amepotea.'

"Edina amepoteza? Ameenda wapi? Kwa nini?" Alijiuliza.

Picha ilikuwa ni ya Edina. Haikuwa ile ya miezi sita iliyopita ambayo ilikuwa ni ya harusi. Ilikuwa ni picha nyingine tofauti.

Akaanza kusoma maelezo yaliyokuwa chini ya picha ile.

'Mwanamke mmoja, Edina Barton, amepotea baada ya kutoweka nyumbani kwa mumewe Dk. Fiston Kabanga.

Edina ana siku ya nne sasa tangu aondoke nyumbani hapo bila taarifa yoyote na mumewe amejaribu kumtafuta maeneo yote imeshindikana. Yoyote atakayemuona, basi awasiliane na mumewe, au kituo cha polisi kilicho karibu naye. Zawadi nono itatolewa."

Tangazo hilo lilimaliziwa na namba za simu za mume wa Edina.' Vyovyote itakavyokuwa, lakini ukweli alioupata Kadili hapo ni kwamba Edina hayupo kwa mumewe kwa sasa.

"Kwa nini? Amepatwa na matatizo gani? Ametekwa na watu wasiojulikana? Amepata ajali na mwili wake umeshindwa kupatikana hadi leo? Au ametoroka mwenyewe?"

Hayo ni mawazo yaliyokuwa aliyokuwa nayo Kadili. "Na kwa nini atoroke wakati ndoa ameitaka mwenyewe na mama yake?" Alijiuliza mwenyewe na hakupata jibu.

Kengele ikagonga kwenye kichwa cha Kadili kuwa kwa hili lililotokea, basi huenda hata yeye lisimuache salama.

**Siku ya tatu ilikuwa imepita. Maisha yalikuwa yakiendelea kama kawaida. Hakukuwa na dalili yoyote ile kama kungekuwa na kitu chochote kibaya mabacho kilitegemewa kutokea kwenye familia ya kina Kadili.**

Kama Edina atakuwa ameuawa au kupata ajali, itakuwa ni simanzi kubwa kwa Kadili kwa sababu ni mwanamke ambaye alimkubali na kumuweka moyoni, licha ya kwamba hakuwahi kupata nafasi ya kumuelezea maswahibu yake ya moyoni.

Utakuwa ni msiba mkubwa kwake. Kama atakuwa ameamua kumtoroka mumewe, basi hata kama atakuwa amekwenda sehemu nyingine, lakini mtu wa kwanza kushukiwa anaweza kuwa ni yeye.

"Edina utaniponza tena Edina. Mama yako anaweza kudhani uko kwangu." Kadili alijikuta akilalamika peke yake.

Akili ilianza kumtuma kuwa kwa siku hizi mbili tatu, aondoke nyumbani kwao na kwenda kuishi sehemu nyingine kwa muda.

Kwa siku hizi, nyumbani kwao utakuwa ni sehemu hatari, kwani watakapokuwa wakimsaka, moja ya sehemu ambayo inaweza eneo sahihi la kutafuta ni nyumbani kwao.

Kama mama yake aliweza kutuma mabaunsa na kufika kwao, wakamchuka na kumpeleka kwake, haitoshangaza sasa akaja na askari kuja kumsaka Edina, ambaye hawatomuona na baada ya hapo, akaweza kuchukuliwa yeye kwa ajili ya kuisaidia polisi, hadi hapo atakapopatikana akiwa hai au maiti yake.

Lakini pia ithibitike kuwa kupatikana kwake huku awe hai au amekufa, hakukuwa na uhusiano wote na yeye, hapo ndipo atakapokuwa huru.

Wazo lingine lilimjia Kadili. Kama akiondoka kwao kwa ajili ya kukimbia tatizo hili, wakija askari na kutomkuta, inaweza kutafsiriwa kuwa yupo pamoja na Edina huko aliko. Yaani inawezekana ikaonekana ni yeye aliyemshawishi au kumsaidia kutoroka. Kwa vyovyote vile, katika hili aliona kuna kitu kinakuja mbele yake, hivyo inambidi awe makini.

Na moja ya tahadhari ni kuchagua ama aondoke nyumbani, au aendelee kukaa. Yote mawili aliyeona ni mazuri na mabaya pia.

Mwisho akaona bora amshirikishe mtu katika hili. Ni nani? Akaamua jambo hili mama yake ndiyo aamue, hivyo ni lazima amwambie kwanza ajue nini kimetokea, ndiyo wajue nini la kufanya.

************************************

Mama Kadili alimuangalia kijana wake kwa makini baada ya kumaliza kusoma gazeti la Nipashe juu ya tukio la kupotea Edina Barton.

"Makubwa, madogo yana nafuu." Alijikuta akisema.

Kadili hakusema kitu chochote zaidi ya kumtazama kwa makini mama yake, akionekana kutaka msaada wake.

"Haya wewe mwenzangu umejipinga vipi?"

"Niondoke"

"Uende wapi? Wakija hapa si ndiyo watasema umetoroka naye au umemtorosha."

"Sasa nifanyeje mama?"

"Kaa hapa hapa, ili kama wale mabaunsa, kama askari wakija wakukute hapa hapa."

"Halafu wanikamate?"

"Bora wakukamate hapa hapa nyumbani, kila mtu anakuona kuwa uko peke yako, mimi mama yako, dada zako, mtaa mzima kwa sababu huko mbele watakosa ushahidi, lakini ukiondoka hapa watauliza kama kweli hajafanya kitendo hicho kwa nini aliondoka kwao?" Mama alijenga hoja nzito.

Kwa kiasi ilionekana kuwa mashiko kwa Kadili, hivyo akaamua kufuata ushauri wa mama yake.

"Sawa mama nimekusikia sitoondoka nitakaa hapa hapa."

"Kwa hili mwanangu mimi mwenyewe nitakutetea mwanzo mpaka mwisho, mtu keshaolewa huko, anakaa na mumewe, wakorofishane atoroke halafu waje kumkamata mwanangu hapa, safari hii tutafikishana mbali, wakitaka wanikamate mimi, siyo wewe." Alimaliza kwa sauti kali ambayo ilionekana kumaanisha kile anachokiongea.

Safari moja kwa moja kwa rafiki yake Meze. Hakumkuta dukani, alimkuta kama mtu aliyekuwa anataka kuondoka.

"Vipi naona leo mtoko."

"Nataka nienda mjini kuna bidhaa zimepungua, ndiyo mjomba wamenituma niende kununua."

"Bwana umepata taarifa yule mtoto katoroka kwa mumewe." Kadili alimwambia mwenzake kwa sauti ya chini kana kwamba hataki mtu mwingine asikie.

"Usiniambie bwana."

"Ndiyo hivyo Meze, hivi mimi hapa nilipo nina wasiwasi kweli."

"Ya nini?"

"We huoni kama ni hatari. Mama yake na wale mabaunsa mtu wa kwanza kumshuku si mimi?"

"Mhh, kweli lakini."

"Mwanangu leo au kesho unaweza kuona mabaunsa nyumbani au askari wakaja kunikamata."

"Sasa umejiandaaje?"

"Mimi nilikuwa nataka kutoroka, lakini mama kaniambia nisiende popote. Kitendo chochote kile cha kuondoka kitasababisha nionekane kweli nimemtorosha."

"Kweli, anachosema mama yako ni sahihi."

"Meze ndugu yangu, kusema kweli huyu mwanamke pamoja na kwamba si mpenzi wangu, lakini amenitesa sana, amenisababishia majanga makubwa na kama hivi nilidhani yameisha lakini ndiyo kwanza yanaanza." Kadili aliongea kwa sauti ya kukata tamaa.

"Hapana, usijilaumu wewe na wala usimlaumu Edina. Huwezi kujua haya yote yanatokea kwa sababu gani."

************************************

Siku ya tatu ilikuwa imepita. Maisha yalikuwa yakiendelea kama kawaida. Hakukuwa na dalili yoyote ile kama kungekuwa na kitu chochote kibaya mabacho kilitegemewa kutokea kwenye familia ya kina Kadili.

Walishangazwa na hilo. Timbwili la mama Pauline wanalitambua vema. Mama anatambua jinsi alivyo mwepesi wa kutuma mabaunsa.

Kadili anajua ubabe, ufedhuli, jauri na ukatili na Mama Pauline. "Inawezekana labda wamempata." Hilo ni wazo ambalo lilimjia Kadili baada ya kuona inapita siku ya tatu na tayari ilishakuwa jioni bila dalili ya askari wala mabaunsa.

"Hodi." Sauti ya ghafla ilisikika na kumshtua Kadili.

Hata hivyo, ilikuwa ni sauti ya mtu ambaye anamfahamu. Ni Meze, hivyo wasiwasi ulipungua.

Akili nyingine ikamjia kuwa huenda akawa ameongozana na watu wengine.

Taratibu alinyanyuka kwenye kochi na kwenda kufungua mlango.

Mikono ilikuwa inatetemeka. Pamoja na yote alitegemea yanayokwenda kutokea. Akafungua.

Itaendelea Jumamosi

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA


**SHAMBA LINAUZWA**, Hekari 25@Tshs 800,000/= ziko Miono Kijiji cha Mkange Wilaya ya Chalinze (kuelekea Sadani Game Reserve) mwendo dakika 40 toka barabara kuu iendayo Tanga. Wasiliana na 0713 604049 / 0784 604049.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### KUPOTEA KWA CHETI



**JUSTINE J. MALEKANO** Mtajwa hapo juu anatangaza kupotelewa na cheti Cha kidato cha Nne chenye namba **S.0989/0052** Kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa kupitia Shule ya sekondari KIBARA mwaka 2016. Kwa atakae kiona atoe taarifa kituo chochote Cha polisi kilichopo Karibu kwa Kumb. **KBR/RB/464/2018.**

115468302

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;207/2019**

**Ombi la ZAMOYONI SAID KIPWASA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SAID KIPWASA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/10/2019

Tarehe 17/10/2019

Sahihi ya Hakimu

115467602

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO

TANGAZO LA KUITWA SHAURINI
SHAURI LA MADAI NAMBA: 363..2014

**Mdai:................................. ASHERI MAHERERE**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: ..........ZAMOYONI MOGERA MAKWIGI**

**Kwa: ZAMOYONI MOGERA MAKWIGI**

**Ombi la Mdai: ASHERI MAHERERE**

**Madai ya: PESA SHILINGI 967,500/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 13 mwezi 11 mwaka 2019 saa 08:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 13 mwezi 06 mwaka 2019.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO.

115467702

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO

TANGAZO LA KUITWA SHAURINI
SHAURI LA MADAI NAMBA: 363..2014

**Mdai:................................. ASHERI MAHERERE**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: ..........ZAMOYONI MOGERA MAKWIGI**

**Kwa: ZAMOYONI MOGERA MAKWIGI**

**Ombi la Mdai: ASHERI MAHERERE**

**Madai ya: PESA SHILINGI 967,500/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 13 mwezi 11 mwaka 2019 saa 08:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 13 mwezi 06 mwaka 2019.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO.

115467802

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**YUSTER JOHN SAMWEL** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye namba za usajili **MC 669 CDQ.** Chassis No. **MD2A21BYXJWJ93600,** Engen No. **PFZWJJ54704.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/285426/2019.**

115467402

---

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KIYUNGA GWANCHELE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 942 BNE** MASSEY YENYE CHASSIS NAMBA **3595243** MODEL FERGUSON KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KHMTR/RB/819/2019.**

115468102

---

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MWANZA
AT MWANZA

APPLICATION NO 47/2019

IN THE MATTER OF A MENTAL HEALTH ACT, ACT NO 21 OF 2008
AND
IN THE MATTER OF APPLICATION OF MANAGEMENT OF ESTATE OF FIDAHUSSEIN JAFFER BANDAL BY MOHAMED RAFIQ BANDALI

**PUBLIC NOTICE**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of management of estates of Fidahussein Jaffer Bandali is made to the above named applicant.

Objections/Caveat to the grant should be filed on or before the 4th of November 2019 of the publication of this Notice in the Gazette.

Given under my hand and of the seal of the Court this 17 day of October 2019.

RESIDENT MAGISTRATE
MWANZA

115467902

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA

SHAURI LA RUFAA JINAI NO 208 LA 2017

**D.P.P...............................APPELLANT**

**DHIDI YA**

1. KUSEKWA S/O JOHN
2. KANSIKILA S/O VIRAHONZA
3. BAHATI S/O MASALU

........RESPONDENTS

**Kwa: kusekwa S/O John na wenzake**
**Popote mlipo.**

**KUITWA SHAURINI**

Mnaarifiwa kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 25/10/2019 kuja kusikiliza rufaa iliyofunguliwa na D.P.P Dhidi yenu.
Mnatahadharishwa kuwa endapo hamtafika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu pamoja na chapa ya mahakama hii leo 11/10/2019

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA

215468002

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA

SHAURI LA RUFAA JINAI NO 215 LA 2017

**D.P.P.......................................APPELLANT**

**DHIDI YA**

1. CHACHA S/O WAMBURA
2. GERARD S/O JAPHARY
3. SAID S/0 JACKSON

.............RESPONDENTS

**Kwa: Chacha S/O wambua na wenzake 2,**
**Popote mlipo.**

**KUITWA SHAURINI**

Mnaarifiwa kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 25/10/2019 kuja kusikiliza rufaa iliyofunguliwa na D.P.P Dhidi yenu.

Mnatahadharishwa kuwa endapo hamtafika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu pamoja na chapa ya mahakama hii leo 11/10/2019

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA

215468002

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA

SHAURI LA RUFAA JINAI NO 186 LA 2018

**D.P.P...................................APPELLANT**

**DHIDI YA**

1. E.933 CPL PHILIMATUS S/O FREDRICK
2. SSP PAUL S/P CUTHBERT MUNG'ONG'O
3. SAID S/O MUSA @SAID
4. MAIG S/O JAMES @MAJANJARA
5. MUNIKO S/O NYAMHANGA@MWITA
6. JONAS S/0 MARWA@CHACHA
7. MWITA S/O WILLIAM @KIMETI
8. ALEX S/O PETER @MABU

.....RESPONDENTS

**Kwa: Chacha S/O wambua na wenzake 7,**
**Popote mlipo.**

**KUITWA SHAURINI**

Mnaarifiwa kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 24/10/2019 kuja kusikiliza rufaa iliyofunguliwa na D.P.P Dhidi yenu.
Mnatahadharishwa kuwa endapo hamtafika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu pamoja na chapa ya mahakama hii leo 11/10/2019

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA

215468002

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

**HASNAIN PYARALI SHIVRAJ** anatangaza kupotelewa na kadi ya **BAJAJ aina ya TVS** KING yenye namba za usajili **MC 650 BYS,** Chassis **No. MD6M14PA3J4D10587,** Engine No. **AK4DJ213254.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **SIN/SIN//RB/345610/2019.**

115467302

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**HATI YA KIAPO**
**(AFFIDAVIT)**

Mimi **MARTIN ROGERS SEMGAYA SEZINGA** mkazi wa Magomeni nikiwa na akili timamu na bila kushawishiwa na mtu yeyote naapa na kuthibitisha haya yafuatayo:

1. KWAMBA mimi **MARTIN ROGERS SEMGAYA SEZINGA** ni mmiliki wa kiwanja **Plot No. 2A, BLOCK O MABAWA TANGA.** Kwa bahati mbaya nimepotelewa na hati ya Offer ya kumiliki ardhi na juhudi ya kuitafuta haijafanikiwa.
2. KWAMBA nimeripoti upotevu huo kituo cha Polisi Magomeni na kupewa Loss Report yenye namba **MAG/RB/3707/2019.**
3. KWAMBA naiomba ofisi yako itambue nilikuwa na hati ya Offer ya kiwanja hicho lakini imepotea. Kwa hiyo ninaomba kupatiwa hati nyingine kwa jina hili la **MARTIN ROGERS SEMGAYA SEZINGA.**

**UTHIBITISHO**
Nathibitisha kuwa yote niliyoyatamka ni ya kweli tupu kwa kadri nijuavyo sheria za viapo.

**MBELE YA: MH. R. KATEMBO**
**CHEO: HAKIMU**

115467202

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**HATI YA KIAPO**
**(AFFIDAVIT)**

Mimi **ROGERS SEMGAYA SEZINGA** mkazi wa Magomeni nikiwa na akili timamu na bila kushawishiwa na mtu yeyote naapa na kuthibitisha haya yafuatayo:

4. KWAMBA mimi **ROGERS SEMGAYA SEZINGA** ni mmiliki wa kiwanja **Plot No. 1A, BLOCK O MABAWA TANGA**. Kwa bahati mbaya nimepotelewa na hati ya Offer ya kumiliki ardhi na juhudi ya kuitafuta haijafanikiwa.
5. KWAMBA nimeripoti upotevu huo kituo cha Polisi Magomeni na kupewa Loss Report yenye namba **MAG/RB/3707/2019.**
6. KWAMBA naiomba ofisi yako itambue nilikuwa na hati ya Offer ya kiwanja hicho lakini imepotea. Kwa hiyo ninaomba kupatiwa hati nyingine kwa jina hili la **ROGERS SEMGAYA SEZINGA.**

**UTHIBITISHO**
Nathibitisha kuwa yote niliyoyatamka ni ya kweli tupu kwa kadri nijuavyo sheria za viapo.

**MBELE YA: MH. R. KATEMBO**
**CHEO: HAKIMU**

115467202

---

### KUPOTEA KWA KADI

**ARMAN MOHAMAD SAIDAN** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN XTRAIL** yenye usajili wa namba **T895 BZC.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/CEN/RB/389692/2019**

115467102

---

THE GOVERNMENT APPOINTED COURT BROKER
MASHANGO INVESTMENT COMPANY LIMITED

**Fredrick Mwaipungu** **03/09/2019**
**..................................**
**KATA YA NKUNGA,**
**S.L.P 148**
**TUKUYU RUNGWE**

**YAH; TAARIFA YA KUACHA KUTUMIA MASHAMBA NA NYUMBA KUONDOKA KATIKA MAENEO HAYO.**

Kwa idhini niliyopewa na baraza la ardhi nyumba na makazi mbeya.
Napenda kuwapa taarifa wahusika wote kuacha kutumia mashamba pamoja na nyumba na kuondoka mara moja.
Taarifa hii ni ya muda wa siku kumi na nne [14 days] kuanzia siku muipatapo taarifa hii
Kushindwa kutekeleza amri hii hatua za kisheria zitafuata dhidi yako.

M.A. MASHANGO
MKURUGENZI
"EXCELLENT SERVICE IS OUR "MOTTO"

**Nakala**
1. **Mtendaji wa eneo**
2. **Mwenyekiti wa eneo**
3. **Mkuu wa kituo cha polisi Tukuyu**
4. **JOSEPH ANYELWISYE**


115468202

---


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# RAIS NAPOLI APANGA KUMUUZA KOULIBALY




**NAPLES,** Italia

RAIS wa Napoli, Aurelio De Laurentiis, amebainisha kwamba utakuja wakati atamuuza mlinzi wake nyota, Kalidou Koulibaly.

Koulibaly amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa walinzi bora kabisa duniani kwa sasa tangu alipojiunga na Napoli akitokea Genk mwaka 2014.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal mwenye umri wa miaka 28, kwa muda mrefu alikuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na Manchester United kabla ya miamba hao wa Ligi Kuu ya England kumsajili Harry Maguire kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia kuwa mlinzi ghali zaidi.

Koulibaly ameendelea kuhusishwa na mpango wa kutua United na wakati alipoulizwa kuhusu mlinzi huyo wa kati wa Napoli, De Laurentiis aliiambia Sky Sport Italia: "Nampenda mno Koulibaly na nilikataa euro milioni 105, lakini kuna muda utafika nitalazimika kumuuza.

"Yeyote anayesema hatujaimarisha safu yetu ya ulinzi hayupo sahihi."

Kiungo wa Napoli, Fabian Ruiz pia amekuwa akihusishwa kutakiwa na klabu kadhaa wakiwamo wapinzani wa Ligi Kuu ya Hspania, La Liga, Barcelona na Real Madrid.

Fabian alijiunga na Napoli akitokea Real Betis kwa euro milioni 30 msimu wa 2018-19 na nyota huyo amekuwa na namba ya kudumu kwa miamba hao wa Serie A.

# Matip: Nipo tayari kuivaa Man United

**LIVERPOOL,** England

MLINZI wa Liverpool, Joel Matip yupo tayari kuwa sehemu ya kikosi cha Jumapili kitakachoivaa Manchester United kama akiitwa.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 28, aliikosa michezo ya ushindi ya Liverpool nyumbani dhidi ya Salzburg na Leicester City kabla ya mapumziko ya mechi za kimataifa baada ya kuumia kwenye mchezo dhidi ya Sheffield United, Septemba 28, mwaka huu.

Hata hivyo, Matip alirudi kwenye mazoezi Jumanne na sasa yupo tayari kuanza kwenye mchezo wa mwishoni mwa wiki wa Ligi Kuu dhidi ya United utakaopigwa pale Old Trafford.

"Nimerudi kwenye mazoezi na nina matumaini nitakuwa fiti," alisema akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Nimerudi kwenye mazoezi na najisikia vizuri. Bila shaka, kama nikihitajika nitakuwa pale.

"Majeruhi huwa yanatokea kwa mchezaji. Sasa nimerudi. Natumaini kubakia na naweza kuwa kwenye mtazamo chanya."

Golikipa, Alisson, ambaye alikuwa nje ya dimba kwa sababu ya majeruhi ya kigimbi alichoumia wakati wakishinda mabao 4-1 dhidi ya Norwich City pia amerudi kwenye mazoezi mapema wiki hii.

Kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kinaongoza msimamo wa Ligi Kuu kwa tofauti ya pointi nane dhidi ya Manchester City.







# Mbappe, Cavani warudi kikosini kuibeba PSG

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain ina habari njema baada ya Kylian Mbappe kurejea kikosini na atakuwa tayari kuivaa Nice, huku Edinson Cavani pia akijumuishwa.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, walikuwa na changamoto ya kikosi chao kukabiliwa na majeruhi wakati wa mapumziko ya mechi za kimataifa, huku Neymar ambaye alisajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia akiwa ameumia na kiungo Idrissa Gueye pia ana maumivu ya misuli.

Lakini kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel jana Ijumaa kilitarajia kumtumia Mbappe kwenye mchezo wa Ligi Kuu.

Mbappe alikuwa nje ya dimba tangu mwanzoni mwa msimu huu na aliachwa kwenye kikosi cha Ufaransa kwenye mechi zake za kimataifa.

Tuchel aliwaambia waandishi wa habari Alhamisi kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, "amefanya mazoezi ya kawaida" na jana alimtarajia kumtumia kwenye kikosi chake.

"Ninafuraha kwamba, tumefikia makubaliano na timu ya Taifa ya Ufaransa kwa sababu hakucheza," alisema Tuchel.

"Jumatatu alifanya mazoezi na alifanya mazoezi ya peke yake ili kumuweka fiti zaidi. Hangeweza kucheza dhidi ya Uturuki."

Mbappe sasa atajiunga kwenye kikosi cha PSG pamoja na anayeshikilia rekodi ya mabao, Cavani, ambaye hajacheza tangu Agosti.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay mkataba wake utamalizika mwishoni mwa msimu huu na anahusishwa na mpango wa kijiunga na Juventus.

HABARI MICHEZO

# Solskjaer kusajili nyota sita Januari

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amepanga kusainisha wachezaji sita wakati wa kipindi cha dirisha dogo la usajili Januari mwakani ili kuimarisha kikosi cha Manchester United.

Kwa mujibu wa Gazeti la Daily Mail, Solskjaer ametoa orodha ya wachezaji sita ambao anapanga kuwanasa ili kufanya marekebisho makubwa kwenye kikosi hicho.

Saul Niguez kiungo wa Atletico Madrid, ameripotiwa kuwa mmoja wa wachezaji hao sita ambao wanaaminika watakapotua tu Old Trafford basi watafanya kikosi hicho kuwa cha kiushindani tena kwenye mikikimikiki ya Ligi Kuu England.

Man United imekuwa na changamoto nyingi msimu huu ikiwa haina uwezo wa kufunga zaidi ya bao moja kwenye mechi na hivyo kujikuta wakishika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England na keshokutwa Jumapili wana mtihani mzito wa kuwakabili Liverpool.

Matokeo ya ovyo, yamewafanya Man United kuweka kwenye rada wachezaji sita inaotaka kuwaongeza kikosini, wakiwamo Saul, kiungo wa Leicester City, James na washambuliaji Mario Mandzukic wa Juventus na Moussa Dembele wa Lyon.

Kikosi hicho kinasaka pia beki wa kati na beki wa kushoto kwa ajili ya kukifanya kuwa imara zaidi licha ya kwamba kwenye dirisha lililopita walifanya usajili wa pesa nyingi walipomnasa beki Harry Maguire.

Kinachosubiriwa ni kuona kama orodha hiyo ya wachezaji wengi watanaswa kwenye dirisha la Januari, huku straika Mandzukic ndiye anayetajwa kwa uhakika mkubwa kwamba atatua Old Trafford katika dirisha hilo la majira ya baridi.





# WENGER ALIVYOMKOSA GRIEZMANN ARSENAL

**LONDON,** England

IMEFICHUKA kwamba, kutofuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2017 ndiko kulikosababisha klabu ya Arsenal kushindwa kumsajili, Antoine Griezmann, kwa mujibu wa ESPN.

Imedai kwamba, Griezmann ambaye sasa ni mchezaji wa klabu ya Barcelona alikuwa kwenye orodha ya wachezaji ambao kocha, Arsene Wenger alikaribia kuwasajili, lakini kikwazo kikawa kutofuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Msimu wa 2016/17, Arsenal walijitahidi kufuzu kucheza michuano hiyo wakati waliposhinda mechi zao zote tano za mwisho wa msimu kwenye Ligi Kuu England, lakini mambo hayakuwa mazuri na hivyo kumaliza pointi moja nyuma ya Liverpool kwenye nafasi ya tano.

Kilichokuwa kimepangwa ni kwamba kama Arsenal ingekamatia tu tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, basi moja kwa moja ilikuwa na nafasi nzuri ya kumchukua Griezmann. Staa huyo alikuwa akisakwa pia na Manchester United.

"Kilichokuwa kimepangwa ni kwamba Arsenal kama wangefuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya wangemsajili Antoine Griezmann, lakini wakashindwa kufanya hivyo kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 20 na hivyo matumaini yao ya kumpata Griezmann yaliishia hapo," ilibainisha taarifa hiyo.

# *Mashabiki waliowabagua England Bulgaria wanaswa*

**SOFIA,** Bulgaria

MASHABIKI watano wa Bulgaria wamekamatwa kwa kosa la kufanyia vitendo vya kibaguzi wachezaji wa timu ya Taifa ya England katika mchezo wa kufuzu michuano ya Euro 2020.

Idadi kubwa ya mashabiki waliwabagua wachezaji wa England wenye asili ya Afrika wakati wa mchezo wao uliochezwa mjini Sofia, Bulgaria.

Mshambuliaji Raheem Sterling alikuwa mhanga wa tukio hilo baada ya mashabiki kumdhihaki kwa kumuita nyani.

Tukio hilo lilisababisha mchezo huo ambao England ilishinda mabao 6-0 kusimama mara mbili baada ya kocha Gareth Southgate kulalamika kwa mwamuzi.

Mashabiki watano walikamatwa na polisi baada ya kufanyika uchunguzi uliowaweka matatani.

Licha ya kutolewa tangazo la kuwataka mashabiki kuacha kuwafanyia vitendo vya kibaguzi wachezaji hao, lakini walivaa fulana za rangi nyeusi zilizokuwa na ujumbe wa kutokubali maagizo hayo.



# DONDO[illegible]OKA MAGAZE[illegible]AYA




# EMERY SASA AKUBALI YAISHE OZIL ARSENAL

**Katika wiki mbili ama tatu zilizopita ameimarika, sasa najisikia vizuri naye, anaweza...**

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery ni mwenye furaha na kuimarika kwa Mesut Ozil katika mazoezi wakati huu kiungo huyo akiendelea kuwa na malengo ya mustakabali wake wa baadaye kuendelea kuwapo hapo Emirates.

**Ozil amecheza mechi mbili tu katika mashindano yotemsimu huu na bado katika mahojiano na The Athletic juzi, Alhamisi alisisitiza hataondoka Arsenal kabla ya mkataba wake kumalizika mwaka 2021.**

Emery pia alionekana kutoa nafasi nyingine kwa Ozil, akifunguka kikwazo cha kupata nafasi finyu msimu huu, wakati huu wakijianda na mechi ya Ligi Kuu keshokutwa, Jumatatu ugenini dhidi ya Sheffield United kwamba ni pamoja na suala lake na Sead Kolasinac la kuvamiwa kwa silaha na kutaka kuibiwa jijini London.

Emery hivi karibuni alidai Ozil hajaonyesha kiwango cha kutosha katika mazoezi ili kujihakikishia nafasi ya kucheza mara kwa mara, lakini amefurahishwa na namna mchezaji huyo alivyojibu.

"Pamoja na Mesut, mwaka huu ulianza kwa ugumu kwake," Emery aliuambia mkutano wa wanahabari Alhamisi. "Katika maandalizi ya msimu mpya kabla, alifanya kazi vizuri na alikuwa akicheza kwenye mechi.

"Bali matatizo yake na Sead kulistisha maendeleo yake na kisha baada ya matatizo hayo, alikuwa mgonjwa kwa wiki moja. Alipoteza muda mwingi wa mazoezi ili kuendelea kuwa fiti.

"Katika wiki mbili ama tatu zilizopita, ameimarika katika mazoezi. Ni vizuri. Sikufunga naye uwezekano wa kucheza. Kama yupo vizuri, kama yupo tayari, kama anapatikana na kujifua, kutupa hisia nzuri kila siku katika mazoezi, anaweza kucheza.

"Wazo langu ni kumtumia kila mchezaji na ni mmoja kikosini ambaye anaweza kutusaidia. Ana uelewa mkubwa na ubora, tutamhitaji katika mechi zijazo.

"Ni mwenye furaha sana kwa namna anavyoimarika, namna anavyojifua kila siku. Ni mchezaji mmoja zaidi kikosini. "[Karibuni] katika kipindi hicho, pengine utimamu wa mwili, labda na wimbo zaidi, labda kutegemeana na kila mechi, kulikuwa na wachezaji wengine mbele yake. Sasa, Ninajisikia vizuri naye."

Kieran Tierney yupo tayari kuanza katika Uwanja wa Bramall Lane keshokutwa, wakati Alexandre Lacazette amerejea kamili mazoezini, na Emery akikataa kuweka kando uwezekano wa straika huyo wa Ufaransa kuanza.

"Leo [juzi] ilikuwa mara yake ya kwanza kujifua nasi na anajisikia vizuri," alisema Emery, akiongeza kuhusu maendeleo ya kuwa fiti kwa Lacazette. "Itategemea namna gani atajisikia katika siku inayofuata endapo atacheza Jumatatu, ila ni chanya. Sijui kama atacheza kwa asilimia 90 ama ataanzia katika benchi."

## ZISIKUPITE

### POGBA, ZIDANE WAKUTANA

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, 26, amekutana na kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane huko Dubai wakati wa mapumziko ya kupisha mechi za kimataifa, kukichochea tetesi zinazomzunguka nyota huyo kuondoka Old Trafford. ***(Mirror)***

### MATIC AWINDWA INTER MILAN

KIUNGO wa Manchester United na Serbia, Nemanja Matic, 31, anatakiwa na Inter Milan. ***(Sun)***

### RAKITIC AICHOMOLEA UNITED

KIUNGO wa Barcelona, Ivan Rakitic, 31, ameweka kando uwezekano kujiunga na Manchester United dirisha la usajili la Januari na familia yake haitaki kwenda kuishi Manchester. ***(Mail)***

### EL CLASICO YANUKIA DECEMBA 7

LA Liga imetoa mapendekezo kwa Shirikisho la Soka la Hispania kuwa ratiba ya mechi ya El Clasico (Barca vs Madrid) ambayo ilikuwa ichezwe Oktoba 26 katika Uwanja wa Camp Nou, badala yake sasa ipigwe Desemba 7, mwaka huu. Tayari waliomba mechi hiyo ikapigwe Santiago Bernabeu jijini Madrid kutokana na kuhofia vurugu za kisiasa. ***(AS)***

### HAALAND AWINDWA CITY

MSHAMBULIAJI wa Red Bull Salzburg, Erling Haaland anawindwa na Manchester City. Mchezaji huyo raia wa Norway mwenye umri wa miaka 19, ni mtoto wa kiungo wa zamani wa Man City, Alf-Inge Haaland. ***(Sun)***

### DEMBELE AMULIKWA EVERTON

MSHAMBULIAJI wa Lyon, Moussa Dembele, 23, anataka kurudi kucheza soka England huku kukiwa na taarifa za kuivutia Everton na Manchester United. Nyota huyo wa zamani wa kimataifa wa Ufaransa U-21, hivi karibuni aliichezea Fulham. ***(Football Insider)***

### LIVER KUMPIGA BEI LALLANA

LIVERPOOL ipo tayari kumuuza kiungo Muingereza Adam Lallana, 31, mwishoni mwa msimu kama ataendelea kubaki hapo. ***(Football Insider)***

### SZCZESNY CHUPUCHUPU UNITED

MANCHESTER United iliulizia kuhusu uwezekano wa kupatikana kwa kipa wa Juventus na Poland ambaye aliwahi kuidakia Arsenal, Wojciech Szczesny, 29, wakati wa majira ya joto kabla ya David de Gea kutia saini mkataba mpya hapo Old Trafford mwezi uliopita. ***(Goal)***

### SPURS, UTD KWA ZAKARIA

TOTTENHAM na Manchester United ni miongoni mwa klabu nyingi ambazo zimetia mguu mbio za kumsajili kiungo wa Borussia Monchengladbach, Mswisi Denis Zakaria, 22. ***(Bild - in German)***

### ERIKSEN ASHUSHWA BAYERN

KIUNGO wa Tottenham, Christian Eriksen, 27, "hatoshi kuichezea" Bayern Munich, ameeleza nguli wa klabu hiyo, Lothar Matthaus. ***(Sport 1, via Standard)***

### ADRIAN AJIFUTUA LANGONI

KIPA wa Liverpool, Adrian, 32, amesema 'Wekundu' hao wana makipa hatari wawili tu yeye na mlinda mlango majeruhi, Mbrazil Alisson Becker, 27. ***(Telegraph)***

HABARI MICHEZO

## Netball wajitoa michuano Afrika

**Na Focus Nicus**

TIMU ya mpira wa Pete ya ['Netball'] ya Tanzania imeshindwa kushiriki michuano ya Afrika iliyoanza kutimua vumbi jana nchini Afrika Kusini kutokana na kukosa fedha za maandalizi pamoja na gharama ya safari na malazi ikiwa katika mashindano hayo, imeelezwa.

Katibu Mkuu wa Chama cha Netiboli nchini, (Chaneta), Judith Ilunda, alimwambia mwandishi wetu kuwa wamelazimika kujitoa katika michuano hiyo kutokana na kukosa kiasi cha Sh. milioni 104 walizokuwa wakihitaji kwa ajili ya maandalizi na gharama za kuisafirisha timu hiyo.

Alisema wamefanya jitihada kwa muda mrefu kwa kutafuta wadhamini wa kuwasaidia kiasi hicho, bila mafanikio licha ya kwamba hata Waziri wa Habari Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk, Harisson Mwakyembe naye kuonyesha jitihada zake za kuhangaika huku na kule ili kuiwezesha timu hiyo kushiriki michuano hiyo.

"Kwanza gharama zilishapungua kutokana na ukweli kwamba tayari tulianza maandalizi wenyewe, hivyo tungepata hata kiasi pungufu kidogo ya hapo tungeweza kushiriki, lakini hadi tunafikia hatua ya kujitoa hatukuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kuisafirisha timu," alisema Ilunda.

## BASSFU yawafunda wasanii Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KATIBU Mtendaji Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamduni Zanzibar (BASSFU), Dk. Omar Abdallah Adam, amewataka wasanii kufuata sheria za baraza hilo sambamba na kujisajili ili kupata fursa zilizopo kupitia ufadhili wa serikali na wadau wengine.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za baraza hilo zilizopo Mwanakwerekwe Unguja, alisema ili kuepuka changamoto zisizo za ulazima ni vyema kufuata sheria ambazo zitamuongoza na kumuepushia vikwazo ili sanaa izidi kuimarika.

Alisema sheria zitakapofuatwa humlinda mtu kwa kutekeleza kile alichoambiwa na kufuata utaratibu ili kupatikana ufanisi katika majukumu yao na kuifanya sanaa kujulikana ndani na nje ya Zanzibar.

"Kila mmoja anapaswa kufuata sheria usipofuata sheria unaruhusu baadhi ya viashiria ambavyo vitaleta athari katika sanaa na kukosekana maendeleo ya sanaa nchini," alisema.

Aidha, alisema fursa zitapatikana ukiwa umeshasajiliwa katika sehemu husika kwani ni njia pekee itakayomuezesha msanii kufanya kazi bila ya kupata usumbufu na kumwezesha kupata maendeleo.

Dk. Omar alieleza wasanii hawanabudi kufuata sheria bila ya shuruti katika kazi zao ili kuwa na ufanisi kwani kunaepusha matatizo mengi pamoja na kuondokana na hofu katika utendaji wao wa kazi.

# KASEJA AELEZA STARS INAPOPOTEA KIMATAIFA

**Na Somoe Ng'itu,** KHARTOUM

KIPA chaguo la kwanza wa timu ya Taifa (Taifa Stars), Juma Kaseja, amesema ili Tanzania iweze kufanya vizuri zaidi katika mashindano mbalimbali ya kimataifa, ni lazima idadi ya wachezaji wanaocheza soka la kulipwa ughaibuni iongezeke.

**Kaseja, golikipa wa zamani wa Moro United, Simba, Yanga, Kagera Sugar, amerejea katika kikosi cha Taifa Stars baada ya kuaminiwa na Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Etienne Ndayiragije akiwa amekaa nje ya kikosi hicho kwa miaka sita.**

Akizungumza na Nipashe jijini hapa, Kaseja, alisema Taifa Stars inapokuwa na wachezaji wengi wanaocheza nje ya Tanzania, inakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kupata matokeo chanya tofauti na ilivyo sasa.

Kaseja alisema pia wachezaji wanapocheza nje ya Tanzania hurejea wakiwa na viwango bora na wanakuwa kwenye nafasi ya kushindana kutokana na kuwa katika kiwango bora baada ya kupata uzoefu kutoka katika ligi nyingine wanazoshiriki.

"Natamani kuona Taifa Stars inakuwa na kina Mbwana Samatta watano, Simon Msuva wanne na Himid Mao wawili, tukipata wachezaji wengi wanaocheza nje, kikosi chetu kitakuwa imara, wachezaji watakuwa na uwezo wa kupambana na timu za nje, ndio jambo linalotusumbua leo hii tukikutana na timu kama Senegal," alisema Kaseja.

Kipa huyo mkongwe alisema kuwa pia wachezaji wa Tanzania wanatakiwa wasikate tamaa, wajitume na kuongeza juhudi kila siku mpaka pale ndoto zao zitakapotimia.

Aliongeza kuwa hakuna jambo lisilowezekana mbele ya mwenyezi Mungu na kinachotakiwa ni wachezaji na nchi kutokana tamaa na kutumia nguvu kwenye kuwekeza katika programu za maendeleo.

"Napenda kuona inafika mahali Tanzania inakuwa na wachezaji wengi wenye uwezo wa kuisaidia Stars kupata matokeo mazuri na si sasa hivi kumtegemea mchezaji mmoja, yaani Samatta akikosekana au akiwa mgonjwa, watu mnakuwa na mawazo kibao, tujiimarishe, tuwe na wigo mpana wa wachezaji," Kaseja aliongeza.

**...ATARAJIA MAKUBWA**

Kaseja aliliambia gazeti hili kuwa, bado anaamini ana nafasi ya kusajiliwa na timu nyingine ya ndani au nje ya nchi kutokana na kiwango kizuri ambacho amekionyesha katika mechi za hivi karibuni akiwa na KMC FC pamoja na Taifa Stars.

Alisema katika maisha yake hajawahi kukata tamaa na anaamini muda sahihi utakapofika, atasajiliwa na timu itakayokuwa imekubali kumlipa dau atakalolitaja.

"Kwa sasa mimi bado ni mchezaji wa KMC, kwa kukaa kwangu nje ya Stars kwa muda mrefu na sasa nimerejea, lolote linawezekana, ama kupata klabu yoyote ya nje au ya ndani ya Tanzania, sina wasiwasi," Kaseja alisema.

Kipa huyu ndiye aliiongoza Taifa Stars ikiiondoa Kenya (Harambee Stars) katika mechi za kusaka tiketi za kuwania kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) na vile vile kuifunga Burundi katika mechi ya kusaka nafasi ya kutinga hatua ya makundi ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia.

Kaseja alipangua penalti mbili ugenini dhidi ya Harambee Stars na nyingine kama hizo walipowakaribisha Burundi kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.




Mshindi wa Bonasi wa mechi 12 kati ya 13 ya Jackpot ya SportPesa wa wiki iliyopita, Willy Ngailo, akikabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. milioni 10.4 na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas (kulia) kufuatia kushinda kiasi hicho. Jackpot ya wiki hii ni Sh. milioni 233.6. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga yaipongeza AS Roma kutumia Kiswahili*

**Na Focus Nicus**

HATUA ya Klabu ya AS Roma ya nchini Italia kuwa klabu kubwa ya kwanza kutoka barani Ulaya kuanzisha ukurasa wake katika mtandao wa kijamii wa Twitter kwa kutumia lugha ya Kiswahili, imepokelewa kwa mikono miwili na Klabu ya Yanga ya jijini Dar es Salaam baada ya kuipongeza.

AS Roma ilizindua rasmi ukurasa huo wa lugha ya Kiswahili Jumatano wiki hii ikiwa na lengo kuu la kuwafikia mamilioni ya mashabiki wake wanaotumia lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, Klabu ya Yanga imekuwa ya kwanza kuwakaribisha AS Roma katika ulimwengu wa Kiswahili kwa klabu za nyumbani baada ya kutupia ujumbe katika mtandao wa kuipongeza.

Katika ukurasa huo wa Kiswahili AS Roma iliandika: "@ASRomaSwahili. Ahsante sana kwa upendo na ushirikiano ambao mmetuonyesha tangu tumezindua ukurasa huu rasmi.

"Ni dhahiri kwamba kwa pamoja tutaendelea kushirikiana na kufurahia pamoja hapa hapa kwa lugha ya Kiswahili. Endelea kuja kwa wingi zaidi."

Yanga nayo ilijibu "@YangaSC 1935. Karibuni sana katika ulimwengu wa Kiswahili@ ASRomaSwahili."

Juzi Rais wa Klabu ya AS Roma, Jim Pallotta alitumia ukurasa wake binafsi wa twitter kuthibitisha kuwa ukurasa huo wa Kiswahili umefunguliwa rasmi.

Michezo
Jumamosi Oktoba 19, 2019
Nipashe



Emery sasa akubali yaishe Ozil Arsenal UKURASA 30



Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Aussems amaliza kazi ya Azam FC

**Na Focus Nicus**

BAADA ya kukamilisha ziara yake ya mechi za kirafiki mjini Kigoma na kurejea jijini Dar es Salaam, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, wamesema tayari wamepata dawa ya kuendeleza vipigo katika ligi hiyo.

Simba inayoongoza ligi hiyo ikiwa kileleni na pointi 12 baada ya kushuka dimbani mara nne, itaikaribisha Azam FC katika Uwanja wa Taifa Jumatano ijayo ikitoka kucheza mechi tatu za kirafiki.

Kwanza ilishinda bao 1-0 dhidi ya wageni wao Bandari FC ya Kenya kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Taifa kabla ya kwenda Kigoma kutoa kipigo kama hicho dhidi ya Mashujaa FC na kisha kutoka sare tasa dhidi ya Aigle Noir ya Burundi mechi zote zikipigwa Uwanja wa Lake Tanganyika.

Mechi hizo zimetoa nafasi kwa Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems kufanyia marekesho kikosi chake ambapo amesema amerekebisha makosa yaliyokuwa yakijitokeza kikosini licha ya kuwa na baadhi ya wachezaji kutokana na wengine kuwa katika majukumu ya timu zao za taifa.

"Nimeangalia baadhi ya vitu katika kikosi changu kwenye mechi zetu tatu ambazo tumecheza za kirafiki. Kikubwa ni kuwa kuna mabadiliko makubwa nimeyaona kwao japo sikuwa na wachezaji ila nilivyoviona na kuvifanyia kazi naona kabisa vinatosha kwa mechi iliyopo mbele yetu," alisema.

Simba itaivaa Azam ikiwa na kumbukumbu ya kuibuka na ushindi wa mabao 4-2 kwenye mechi ya Ngao ya Jamii.

# Niyonzima kimeeleweka Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

## Dk Msolla amwachia mpini Zahera aamue moja kabla ya kumwaga wino rasmi, lakini...

HATIMAYE Kiungo fundi mwenye pasi nyingi za kufika, Mnyarwanda Haruna Niyonzima, sasa ni muda tu unasubiriwa kufika na Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera kuamua moja kabla ya kurejea rasmi kuitumikia klabu hiyo ya Mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

**Niyonzima aliyeibukia Rayon Sports na kuichezea kuanzia mwaka 2006–2007 kabla ya kutua APR mwaka 2007–2011 kisha kujiunga na Yanga kuanzia 2011–2017, kwa sasa anaitumikia A.S Kigali ambayo alijiunga nayo akitoka kuitumikia Simba alipodumu kuanzia mwaka 2017–2019.**

Baada ya taarifa kuzagaa kuwa kiungo huyo wa kimataifa wa Rwanda anataka kurejea kuitumikia Yanga, hatimaye uongozi wa klabu hiyo ya Jangwani jijini Dar es Salaam umethibitisha rasmi.

Akizungumza na mwandishi wetu, juzi, Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, alisema ni kweli ameonana na kuzungumza na Niyonzima ambaye ameeleza nia yake ya kurejea kwa mara nyingine kuitumikia klabu yao.

"Ni kweli nilipokuwa Rwanda kikazi wiki iliyopita nilimpigia simu Niyonzima nikamueleza hoteli nilipo kwa lengo tu la kutaka kuonana naye kumsalimia, hata hivyo aliniambia mwalimu tayari nimekusoma kwenye mitandao najua upo hapa,".

"Alipofika tulizungumza na kunieleza yupo tayari kurudi Yanga," alisema Dk. Msolla. Alisema hawezi kutolea uamuzi suala hilo kwa kuwa hilo ni jukumu la Kocha Mkuu, Zahera kutazama mchezaji anayemhitaji na kama akiona Niyonzima ana nafasi katika kikosi chake basi watafanya mchakato wa kumsajili.

"Tusubiri dirisha dogo lifunguliwe, endapo kocha atahitaji kuboresha kikosi chake na kuamua kama Niyonzima anamhitaji hapo ndipo tunaweza kufanya uamuzi," alisema Dk. Msolla.

Yanga kwa sasa ipo jijini Mwanza ikijiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mbao FC Jumanne wiki hii kabla ya kuikaribisha Pyramids ya Misri kwenye mchezo wa mchujo kuwania kushiriki hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga iliyoangukia hatua hiyo baada ya kutolewa raundi ya kwanza na Zesco United kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, itaikaribisha Pyramids Jumamosi ijayo Oktoba 27 kabla ya kurudiana wiki mbili zijazo nchini Misri.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >